**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026


**Dkt. SAADA MKUYA SALUM,**

**WAZIRI WA NCHI-OFISI YA RAIS,**
**FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR**


**JUNI, 2025**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kuwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2. **Mheshimiwa Spika,** ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Waziri mwenye dhamana ya kuisimamia sekta ya fedha na mipango. Kwa unyenyekevu mkubwa ninamshukuru sana kwa imani hiyo aliyonayo kwangu.

3. **Mheshimiwa Spika,** ninapenda pia kumshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Nane ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma mbalimbali za kijamii na kuijenga nchi yenye mazingira mazuri kimaendeleo.

4. **Mheshimiwa Spika,** namshukuru, **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla,** Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia utendaji wa Serikali na kuwatumikia wananchi. Usimamizi na maelekezo yake yamekuwa ni chachu katika utendaji wa Serikali na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid,** Spika wa Baraza la Wawakilishi na **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma,** Naibu Spika kwa kuliongoza Baraza kwa umahiri mkubwa kwa kushirikiana na Wenyeviti wa Baraza.

6. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kutoa shukrani zangu za kipekee kwa Kamati ya Kudumu ya Bajeti inayoongozwa na **Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma** kwa ushirikiano wao katika kuhakikisha ofisi yetu inatimiza azma ya Serikali ya kuwahudumia wananchi. Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2025/2026,** maoni na ushauri wao umezingatiwa katika bajeti hii ninayoiwasilisha leo.

7. **Mheshimiwa Spika,** aidha, ninayo furaha kubwa kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, **Mheshimiwa Juma Makungu Juma**, Mwakilishi wa Jimbo la Kijini ambaye tumeshirikiana naye kutekeleza majukumu ya sekta. Vilevile, nampongeza Katibu Mkuu, **Dkt. Juma Malik Akil,** Naibu Katibu Mkuu Ndugu **Aboud Hassan Mwinyi,** Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango **Dkt. Rahma Salim Mahfoudh** na **Wakurugenzi wote wa Ofisi pamoja na Wakurugenzi wa Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Ofisi yetu**, kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa ipasavyo. Pia, ninawashukuru Wenyeviti wa Bodi za taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango na watumishi wote kwa ushirikiano na kujituma katika kutekeleza majukumu yao.

8. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kutumia fursa hii kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango yenye sehemu kuu tano (5) kama ifuatavyo:- Utangulizi; Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/25; Changamoto na Hatua zilizochukuliwa; Vipaumbele na Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

## B. MAFUNGU YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO

9. **Mheshimiwa Spika,** Kimuundo Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imejumuisha mafungu makuu (7) ambayo ni Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (F01), Mfuko Mkuu wa Serikali (F02), Tume ya Mipango (F03), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04), Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05), Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (F06) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (F07).

10. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango inasimamia taasisi saba (7) zinazojitegemea ambazo ni Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA) na Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi (ZIAAT). Vile vile, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi itasimamia (mipango na kibajeti) Kampuni ya Sukuk (Zanzibar Treasury Sukuk 1 Company Limited) na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (ZIFA).

## C. MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO

11. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imepangiwa kutekeleza miongoni mwa majukumu yafuatayo:-

    i. Kusimamia mapato ya Serikali kutokana na vyanzo mbali mbali yanayojumuisha mapato ya kodi na yasiokuwa ya kodi, misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

    ii. Kusimamia mali za Serikali kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za Serikali pamoja na Hisa za Serikali katika Mashirika na Kampuni ambazo Serikali inamiliki;

    iii. Kusimamia Fedha za Umma, shughuli za Uhasibu na Ukaguzi Serikalini. Katika jukumu hili Ofisi inasimamia Bajeti ya Serikali, usimamizi wa Hazina, huduma za Uhasibu na Ukaguzi wa ndani;

iv. Kusimamia Deni la Taifa kwa kujadili, kushauri na kufuatilia mwenendo wa Deni la Taifa (Mikopo ya Ndani na Nje) na udhibiti wake;

v. Kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha, inayohusisha masuala ya Benki, Bima, Hifadhi ya Jamii na Taasisi zenye kutoa huduma Ndogo za fedha;

vi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye mipango ya kipindi cha muda wa kati kwa kuzingatia idadi ya watu na mahitaji yake;

vii. Kuratibu na kusimamia maendeleo ya uchumi kupitia sekta za kiuchumi na kijamii;

viii. Kuratibu sera za kitaifa na kisekta za kukuza ustawi wa wananchi kwa kubadilisha hali za maisha kupitia rasilimali zilizopo;

ix. Kusimamia upatikanaji na utoaji wa takwimu rasmi kwa maendeleo ya nchi;

x. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya kitaifa na kimataifa; na

xi. Kusimamia na kuendeleza tafiti za kimkakati.

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI HADI KUFIKIA MACHI 2025 MWAKA WA FEDHA 2024/2025

12. **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango ya Mwaka 2025/2026, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 -Machi, 2025) kama ifuatavyo:

13. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango utekelezaji wake umegawika katika maeneo makuu manne (4), maeneo hayo ni:

i. Mapato yanayokusanywa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (F01), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04), Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (F07);

ii. Utekelezaji wa matumizi yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (F01), Mfuko Mkuu wa Serikali (F02), Tume ya Mipango Zanzibar (FO3), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04), Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05), Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (F06) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (F07);

iii. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais -Fedha na Mipango; na

iv. Utekelezaji wa Taasisi zilizosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango.

**Ukusanyaji wa Mapato**

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ilikadiriwa kukusanya **TZS 4,901.691 bilioni** ambayo ni ongezeko la asilimia **77** ikilinganishwa na makadirio ya **TZS 2,767.839 bilioni** ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mapato hayo yamejumuisha mapato katika mafungu ya F01, F04, F05 na F07 hadi kufikia Machi, Ofisi imekusanya **TZS 2,046.780 bilioni** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya **TZS 3,195.705 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

15. **Mheshimiwa Spika,** sababu kubwa ya kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji mapato ni pamoja na kuchelewa kupatikana kwa fedha za washirika wa maendeleo na mkopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa Mapato hayo kwa mafungu ni kama ifuatavyo:-

**Mapato Fungu F01 (Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango)**

16. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai - Machi 2025, Fungu F01 limekusanya **TZS 1,500.493 bilioni** sawa na asilimia **85** ya makadirio ya **TZS 1,771.803 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mapato hayo yamejumuisha mapato ya kodi, mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na mapato yasiokuwa ya kodi. Mchanganuo wa vyanzo vya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) **TZS 667.779 bilioni;**

ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar imekusanya **TZS 473.319 bilioni;**

iii. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo **TZS 277.374 bilion**i; na

iv. Mapato yasiyokuwa ya kodi **TZS 82.022 bilioni** mapato hayo ni Mapato ya Uhamiaji, ununuzi wa magari, ada ya ukodishwaji wa ukumbi, ada ya matumizi ya nyaraka, matangazo, usajili wa wazabuni na Ada ya mafunzo.

**Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)**

17. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2025, Ofisi imekusanya **TZS 0.063 bilioni** sawa na asilimia **65** ya makadirio ya **TZS 0.097 bilioni** ya kipindi cha tathmini ambapo vyanzo vyake ni Vibali vya Utafiti (**TZS 0.037 bilioni**); na Ukodishwaji wa Kumbi za Mikutano ni **TZS 0.026 bilioni.**

**Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali)**

18. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2025, Ofisi imekusanya **TZS 537.352 bilioni** sawa na asilimia **38** ya makadirio ya **TZS 1,412.097 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Upungufu huu wa mapato umetokana na kuchelewa kupatikana kwa mkopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo pamoja na kuchelewa kukamilika kwa

masoko. Hata hivyo, mapato hayo yanatarajiwa kupatikana katika robo ya nne ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Mchanganuo wa vyanzo vya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Mapato ya Wafanyakazi (PAYE) ni **TZS 15.750 bilioni**

ii. Mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **TZS 237.900 bilioni**

iii. Misaada ya Kibajeti (GBS) ni **TZS 76.578 bilioni**

iv. Hati Fungani ni **TZS 179.77 bilioni,**

v. Mapato mengine (mabuku stakabadhi na michango kutoka Taasisi za Serikali) ni **TZS 13.85 bilioni,**

vi. Gawio la kutoka Benki Kuu ya Tanzania ni **TZS 13.500 bilioni.**

**Fungu F07 (Ofisi ya Msajili wa Hazina)**

19. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2025, Ofisi imekusanya **TZS 8.871 bilion**i sawa na asilimia **76** ya makadirio ya **TZS 11.707 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mchanganuo wa vyanzo vya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Gawio la Mashirika ni **TZS 8 bilioni;**

ii. Kodi ya Bohari ni **TZS 0.170 bilioni;**

iii. Uuzaji wa vifaa vikongwe ni **TZS 0.675 bilioni;** na

iv. Kodi za majengo yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ni **TZS 0.026 bilioni.**

**Matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango**

20. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Machi 2024/25, matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango yamefikia **TZS 589.161 bilioni** sawa na asilimia **76** ya makadirio ya **TZS 770.826 bilioni** katika kipindi cha tathmini (Julai-Machi, 2024/25). Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo:

i. Matumizi ya mishahara ni **TZS 48.822 bilioni;**

ii. Matumizi ya uendeshaji wa mafungu ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ni **TZS 31.919 bilioni;**

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ni **TZS 282.396 bilioni;**

iv. Ruzuku zilizopatiwa Taasisi za Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ni **TZS 22.220 bilioni;** na

v. Matumizi ya miradi ya maendeleo ni **TZS 201.240 bilioni** (ambapo **TZS 180.374 bilioni** zimetoka Serikalini na T**ZS 20.866 bilioni** zimetoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**21. Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa utekelezaji wa bajeti kwa mafungu yaliyopo Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ni kama ifuatavyo: -

**Fungu F01 (Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango)**

**22. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu F01, yamejumuisha Programu kuu tatu (3) ndani yake zinajumuisha Programu Ndogo nane (8). Hadi kufikia Machi 2025, Fungu hili limetumia **TZS 276.812 bilioni** sawa na asilimia **68** ya makadirio ya **TZS 407.544 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mchanganuo ni kama ufuatavyo: -

**PF 0101-Programu Kuu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma**

**23. Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali, hadi kufikia Machi 2025, Programu hii imetumia **TZS 51.784 bilion**i sawa na asilimia **43** ya makadirio ya **TZS 121.434 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha Programu Ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali imetumia **TZS 30.504 bilioni** sawa na asilimia **31** ya makadirio ya **TZS 99.115 bilioni** ya kipindi cha tathmini;

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Rasilimali za Nje imetumia **TZS 0.322 bilioni** sawa na asilimia **47** ya makadirio ya **TZS 0.688 bilioni** ya kipindi cha tathmini; na

iii. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi imetumia **TZS 20.958 bilioni** sawa na asilimia **97** ya makadirio ya **TZS 21.631 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizi zimejumuisha ruzuku za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango (ZRA na ZIAAT) ambazo ni **TZS 20.655 bilioni.**

**24. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza pamoja na shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya majadiliano baina Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mgao wa fedha za mradi wa SCALE ambao utaiwezesha Zanzibar kupata **TZS 1.2 bilioni** kwa ajili ya uanzishwaji wa kitengo cha Usimamizi wa Fedha za Kupunguza Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi;

ii. Kukamilisha majadiliano kuhusu mkataba wa Mradi wa Usalama wa Maji kutoka Ofisi ya Shirika la GIZ Dar Es Salaam ambao utaiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupata **Euro 25 Milioni** kwa kutekeleza miundombinu ya maji kisiwani Pemba kwa maeneo ya Kangani, Ole, Pandani na Madenjani.

iii. Kufanya majadiliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea ambapo miradi mitatu yenye thamani ya **USD 548 milioni** ilijadiliwa ambayo ni Ujenzi wa Barabara (km 246), Ujenzi wa Kumbi za Mikutano za Kimataifa (MICE) kwa awamu ya kwanza na Ujenzi wa Bandari ya Wete pamoja na Benki ya Dunia kupitia mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Usalama wa Chakula (TASFAM) ambapo Zanzibar inatarajiwa kupata **USD 41 milioni.**

iv. Kujadili ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 pamoja kwa kutayarisha Hadidu Rejea na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Bajeti ya inayozingatia Masuala ya Kijinsia.

v. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2023/2024 kwa kushirikiana na UNICEF. Wizara zilizofuatiliwa ni Elimu na Mafunzo ya Amali, Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Kilimo, Umwagiliaji na Maliasili, Uchumi wa Buluu na Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa lengo la kuimarisha upangaji na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

vi. Kuandaa Muongozo wa Bajeti ya Serikali (Budget Guideline) ya mwaka 2025/2026 kwa lengo la kutoa maelekezo juu ya utaratibu wa kufuatwa na Wizara/Taasisi za Serikali, kuandaa Jukwaa la Uchumi na Bajeti kwa Vijana, Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya kukusanya maoni katika maandalizi ya bajeti ya mwaka 2025/2026.

vii. Kufanya mapitio na kukamilisha Sheria na Kanuni ya Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu kwa lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

viii. Kushiriki katika majadiliano ya mkataba wa kuondoa utozaji kodi mara mbili baina ya SMZ na SMT, kufanya uchambuzi kuhusu masuala ya utekelezaji wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) pamoja na Mkutano wa Jukwaa la Utulivu wa Kifedha (Tanzania Financial Stability Forum) na Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kodi.

ix. Kukamilisha Dhana ya awali (Concept Note) ya kutafuta Mshauri Elekezi wa kuandaa uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji (Zanzibar Investment Bank) kwa lengo la kurahisisha masuala ya uwekezaji.

x. Ripoti ya Upembuzi Yakinifu juu ya Uanzishwaji wa Soko la Hisa Zanzibar (Zanzibar Securities Market) imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa Serikalini ifikapo mwezi Juni, 2025.

***PF0102-Programu Kuu ya Usimamizi na Sera za Ununuzi na Masuala ya Sheria***

**25. Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu hii ni kuandaa na kusimamia Sera za Ununuzi pamoja na kuandaa mazingira bora ya kazi katika masuala ya kisheria. Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii imetumia **TZS 2.119 bilioni** sawa na asilimia **56** ya makadirio ya **TZS 3.761 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha Programu Ndogo mbili ambazo ni:

i. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Sera za Ununuzi imetumia **TZS 2.030 bilioni** sawa na asilimia **58** ya makadirio ya **TZS 3.496 bilioni,** fedha hizi zinajumuisha fedha **TZS1.566 bilioni** za ruzuku ya ZPPRA; na

ii. Programu Ndogo ya Huduma za Kisheria za Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imetumia **TZS 0.089 bilioni** sawa na asilimia **33** ya makadirio ya **TZS 0.266 bilioni** kwa kipindi cha tathmini.

**26. Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Usimamizi na Sera za Ununuzi na Masuala ya Sheria imetekeleza miongoni mwa shughuli zifuatazo: -

i. Kukamilisha utungaji wa Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma Nambari 2 ya Mwaka 2025, kuendelea kuandaa Kanuni za Sheria hiyo pamoja na kufanya mapitio ya Sheria nambari 12 ya Mwaka 2016 ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

ii. Kuandaa mikataba mbalimbali ikiwemo mkataba kwa ajili ya mkopo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa **TZS Bilioni 50** baina ya Serikali na Benki ya Stanbic;

iii. Kuratibu kikao kimoja (01) cha Kamati ya Majadiliano ya Serikali (GNT);

iv. Kuratibu vikao vya malalamiko ya kodi na mijadala ya kodi ambapo hadi kufikia Machi 2025, Bodi ya Rufaa za Kodi

imekamilisha usikilizwaji wa mashauri 88 kati ya 97 yaliyokuwepo ambapo **TZS 18.230 bilioni** imeamuliwa zilipwe kama kodi ya Serikali;

v. Kuratibu vikao vya malalamiko ya kodi kupitia Baraza la Rufani za Kodi Zanzibar ambapo jumla ya kesi 9 zimesikilizwa kati ya hizo kesi 7 zimekamilika na kuzitolea maamuzi kuwa **TZS 1.5 bilioni** imeamuliwa zilipwe kama kodi ya Serikali na kesi mbili (2) zinaendelea kusikilizwa;

vi. Kuandaa mfumo wa daftari la usajili wa watumishi wa kada ya ununuzi; kwa sasa tunasubiri kupata kibali kutoka Mamlaka wa Serikali mtandao ambao ni wasimamizi wa mifumo yote ya Serikali; na

vii. Rasimu ya Sera ya Ununuzi wa Umma imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa kwa wadau kuanzia mwezi Juni, 2025.

***PF0103– Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango***

**27. Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kuimarisha uendeshaji wa shughuli za Sekta ya Fedha. Hadi kufikia Machi 2025, Programu hii imetumia **TZS 222.909 bilioni** sawa na asilimia **79** ya makadirio ya **TZS 282.349 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha Programu Ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ambayo hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 26.985 bilioni** sawa na asilimia **90** ya makadirio ya **TZS 29.985 bilioni.**

ii. Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti imetumia **TZS 195.084 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya **TZS 250.416 bilion**i kwa kipindi cha tathmini. Fedha hizi zimejumuisha fedha za miradi ya maendeleo **TZS 194.862 bilioni** na fedha za uendeshaji wa Idara **TZS 0.222 bilioni**; na

iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Pemba, imetumia **TZS 0.84 bilioni** sawa na asilimia **43** ya makadirio ya **TZS 1.948 bilioni** kwa kipindi cha tathmini.

**28. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizo zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kusimamia na kuwapatia haki zao wafanyakazi ambapo wafanyakazi **62** wamepatiwa likizo zao za kawaida, **91** wamepatiwa nyongeza ya mwaka, **22** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu na 38 wamepatiwa mafunzo muda mfupi;

ii. Katika kuimarisha mazingira ya kazi, ofisi imefanya ununuzi wa vifaa mbalimbali ikiwemo vya kuandikia, mashine za ofisi, kompyuta na mashine za kudurufu pamoja na kufanya matengenezo ya kawaida ya gari 13 za Ofisi;

iii. Kuratibu vikao vya SMZ na SMT yenye lengo la kuimarisha mashirikiano, mikutano ya mashirikiano ya kikanda ya EAC na SADC pamoja na mikutano ya ndani ya nchi;

iv. Kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Kiuchumi na Kijamii hapa Zanzibar (Zanzibar Research Centre for Social Economic and Policy Analysis -ZRCP) katika kufanya utafiti wa **"Njia za Kuboresha Upatikanaji wa mikopo kwa Taasisi Ndogo Ndogo za Kifedha"** kwa ajili ya kukuza ukuaji wa makampuni ya wajasiriamali ndani ya sekta ya utalii Zanzibar;

v. Muongozo wa Viashiria Hatarishi (Risk Management Framework) umekamilika, hatua inayofuata ni utekelezaji;

vi. Ripoti ya Tathmini ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imekamilika na hatua inayofuata ni kuanza matayarisho ya mpango mkakati mpya;

vii. Kufanya ufuatiliaji wa Programu na miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango ambapo miradi mitatu imekamilika ikiwemo Ofisi ya Mufti, Ujenzi wa Nyumba za Mombasa na Jengo la Mkurugenzi wa Mashtaka;

viii. Kutoa mafunzo tofauti kwa watendaji **47** kwa upande wa Pemba katika eneo la Akili Mnemba (Artificial Intelligence), Mwongozo wa Uchakataji Takwimu za Fedha za Serikali (GFSM 2014) na kujenga uelewa katika kazi za kila siku; na

ix. Kufanya ukaguzi kwa kushirikiana na ZAECA ya kupitia taasisi zinazotoa huduma Ndogo za fedha na kubaini uwepo wa taasis zinazotoa huduma kinyume na taratibu.

**Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali)**

29. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali, hadi kufikia Machi 2025, **TZS 284.600 bilioni** zimetumika sawa na asilimia **88** ya makadirio ya kutumia **TZS 323.862 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Fedha hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kulipa Hati Fungani, Riba ya Hati Fungani na Mikopo ya ndani **TZS 137.083 bilioni;**

ii. Kulipa mafao ya Kiinua Mgongo **TZS 26.406 bilioni** kwa wastaafu 872 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iii. Kulipa Pencheni **TZS 34.821 bilioni** kwa wastani wa wastaafu 13,110 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iv. Kulipa Pencheni Jamii **TZS 14.420 bilioni** kwa wastani wa wazee 31,256 waliofikia miaka 70;

v. Kulipa mishahara **TZS 2.207 bilioni** ya Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

vi. Kulipa matumizi mbali mbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar **TZS 69.663 bilioni.**

**Fungu F03 (Tume ya Mipango Zanzibar)**

30. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu (F03) yanajumuisha Programu kuu tatu (3) ndani yake kuna Programu Ndogo saba (7). Hadi Machi 2025, Fungu limetumia **TZS 5.982 bilioni** sawa na asilimia **59** ya **TZS 10.125 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mchanganuo wa matumizi kwa Programu kuu ni kama ifuatavyo:-

***PF0301-Programu Kuu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi***

31. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kuimarisha uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mipango hiyo. Hadi Machi 2025, Programu hii imetumia **TZS 3.686 bilioni** sawa na asilimia **55** ya makadirio ya **TZS 6.680 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii inajumuisha Programu Ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Kupambana na Umasikini **TZS 2.58 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya **TZS 3.304 bilioni** ya kipindi cha tathmini;

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu **TZS 0.266 bilioni** sawa na asilimia **32** ya makadirio ya **TZS 0.829 bilioni** ya kipindi cha tathmini; na

iii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Ufuatiaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo **TZS 0.839 bilioni** sawa na asilimia **33** ya **TZS 2.547 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

32. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ukusanyaji wa maoni kwa ajili ya kupata Mpango Mpya wa Maendeleo wa muda wa kati (ZADEP) uliofikia ukomo na kuandaa Mpango wa Maendeleo mpya (ZADEP 2026 – 31);

ii. Kuratibu zoezi la ukusanyaji wa maoni ya Dira Mpya ya Taifa ya mwaka 2050 kwa wananchi wa Zanzibar;

iii. Kuimarisha Mfumo Jumuishi wa Uandaaji na Usimamizi wa Mipango na Miradi ya Maendeleo Zanzibar (ZiPS) kwa lengo la kuunganisha mifumo wa kidigital wa ZiPS na mifumo mengine, ambapo watendaji wa Serikali walijengewa uelewa na kupatiwa akaunti za kuingiza taarifa za Taasisi zao;

iv. Kuandaa Mkakati wa Mapendekezo ya Utayari wa Zanzibar kuwa mwenyeji wa miongoni mwa mechi za Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika (AFCON) 2027;

v. Kuwasilisha Maandiko ya Awali (Concept Notes) ya Miradi ya Maendeleo ishirini na mbili (22) kwa ajili ya kupatiwa fedha za kuitekeleza;

vi. Kujadili Mpango Mkuu wa usimamizi wa taka ngumu, utafiti wa upangaji na uwekaji wa mfumo wa usafiri wa umma unaotumia umeme Zanzibar, mapitio ya muundo mpya wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (PSSN III) ikiwemo mapendekezo ya bajeti tengefu pamoja na Mkakati wa upatikanaji wa fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

vii. Kufanya uhakiki wa fidia za mali za wananchi waliopisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbali mbali ikiwemo Binguni, Ukongoroni, Charawe, Kinduni, Kidoti, Makunduchi, Kianga, Dole, Mwakaje, Masingini, Jambiani, Uroa, Kisiwandui, Barabara ya Mtoni –Kinazini, Mgeni Haji, Machui kwa Unguja, Chake Chake – Wete, Ukutini – Mtangani na Vitongoji – Pemba; na

viii. Kufanya uhakiki wa taarifa za daftari la Shehia kwa kutumia teknolojia (Geographical Information System), ambapo majengo **19,855** katika Shehia **40** za Wilaya ya Mjini yameingizwa katika mfumo wa Shehia Register.

**PF0302-Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti**

33. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kusimamia sera za kiuchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa vya Tafiti zitakazosaidia ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu. Hadi Machi 2025, Programu imetumia **TZS 0.699 bilioni** sawa na asilimia **55** ya makadirio ya **TZS 1.270 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii inajumuisha Programu Ndogo mbili ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu iliyotumia **TZS 0.293 bilioni** sawa na asilimia **66** ya makadirio **TZS 0.456 bilioni** ya kipindi cha tathmini; na

ii. Program Ndogo ya Utafiti na Ubunifu iliyotumia **TZS 0.407 bilioni** sawa na asilimia **50** ya **TZS 0.814 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

34. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ripoti tisa za hali ya mfumko wa bei na ripoti tatu za mwenendo wa hali ya kiuchumi zimejadiliwa na kutolewa mapendekezo yatakayopelekea kupungua kwa mfumko wa bei;

ii. Mapitio ya kuimarisha modeli ya kiuchumi ya "Financial Programming" (FP) yamefanyika kwa ajili ya kutoa mwelekeo wa hali ya Uchumi (2025); na

iii. Utafiti wa kuliimarisha, kuliendeleza na kulinusuru Zao la Karafuu kwa Ushirikiano na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (ZARI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) unaendelea. Katika Utafiti huo wakulima 865 na masheha 145 kwa Unguja na Pemba wamehojiwa, vile vile taarifa za udongo ziko maabara kwa uchunguzi.

***PF0303-Programu Kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango***

35. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Hadi Machi 2025, Programu imetumia **TZS 1.596 bilioni** sawa na asilimia **73** ya makadirio ya **TZS 2.175 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Programu hii inajumuisha Programu Ndogo mbili ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar imetumia **TZS 1.264 bilioni** sawa na asilimia **71** ya **TZS 1.776 bilioni** ya kipindi cha tathmini

ii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango Pemba imetumia **TZS 0.332 bilioni** sawa na asilimia **83** ya **TZS 0.399 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

36. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ununuzi wa vitendea kazi, samani za ofisi, vifaa vya kuandikia na vya kielektroniki ili kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi;

ii. Kupatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi watano (5), muda mfupi kwa wafanyakazi wanne (4) na mafunzo ya ndani yametolewa kwa wafanyakazi 55;

iii. Uratibu wa kutengeneza Mkakati wa Usalama Barabarani umefanyika pamoja kutekeleza maagizo yaliyoelekezwa katika Kikao cha Tume ya Mipango juu ya utekelezaji wa Mkakati huo;

iv. Kuratibu shughuli za Ofisi kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana na Ofisi Kuu Unguja katika kusimamia Miradi ya Maendeleo na Ufuatiliaji wake pamoja na kushiriki vikao kazi.

**Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)**

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Fungu F04 limetumia **TZS 5.878 bilioni** sawa na asilimia **59** ya makadirio ya kutumia **TZS 9.884 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu Kuu zifuatazo:-

***PF0401-Programu Kuu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii***

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuongeza ubora na wingi wa takwimu kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Programu hii hadi Machi 2025, imetumia **TZS 4.638 bilioni** sawa na asilimia **69** ya makadirio ya kutumia **TZS 6.677 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii kuu imejumuisha Programu Ndogo mbili:-

i. Programu Ndogo ya Ukusanyaji, Uchambuzi na Uwasilishaji wa Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii. Programu hii imetumia **TZS 3.751 bilioni** sawa na asilimia **68** ya makadirio ya kutumia **TZS 5.502 bilioni** ya kipindi cha tathmini; na

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Kitakwimu katika Mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar. Programu hii imetumia **TZS 0.888 bilioni** sawa na asilimia **76** ya makadirio ya kutumia **TZS 1.175 bilioni** kwa kipindi cha tathmini.

39. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa jumla ya ripoti **45** na kusambazwa kwa wadau kwa njia ya Tovuti, machapisho na Vyombo vya Habari. (Ripoti hizo zinajumuisha; Takwimu za Faharisi ya Bei ya Mlaji, Takwimu za Wageni Wanaoingia Nchini, Takwimu za Uagiziaji na Usafirishaji wa Bidhaa, Takwimu za matukio ya Ajali na Makosa Barabarani,

pamoja na ripoti ya Takwimu za Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto);

ii. Kuendelea kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (Food and Agriculture Organization) kwa matayarisho kazi za ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa Kilimo awamu ya pili; na

iii. Kuratibu vibali vya tafiti **510** kati ya hivyo **448** vilitolewa kwa wanafunzi, vibali 30 vilitolewa kwa Taasisi za Serikali, Vibali 3 vilitolewa kwa Taasisi binafsi, Vibali 3 vilitolewa kwa Watafiti wa kujitegemea na vibali 26 vilitolewa kwa Wageni.

***PF0402-Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***

**40. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Utawala na Uendeshaji hadi Machi 2025 imetumia **TZS 1.24 bilioni** sawa asilimia **39** ya makadirio ya kutumia **TZS 3.207 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu kuu hii imejumuisha Programu Ndogo mbili nazo ni:-

i. Program Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 0.937 bilioni** sawa na asilimia **33** ya makadirio ya **TZS 2.849 bilioni**; na

ii. Program Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Kitakwimu Pemba imetumia **TZS 0.303 bilioni** sawa na asilimia **85** ya makadirio ya **TZS 0.358 bilioni.**

**41. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuwapatia likizo watumishi **31**.

ii. Ofisi iliratibu mafunzo ya kufanya tathmini ya upimaji utendaji kazi kwa wafanyakazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; na

iii. Kusimamia matumizi ya uendeshaji kupitia huduma mbali mbali zikijumuisha maji, usafi, umeme na mawasiliano pamoja na vifaa vya kuandikia, mafuta na samani mbali mbali za Ofisi.

**Fungu F05 (Ofisi ya Muhasibu Mkuu wa Serikali)**

42. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Muhasibu Mkuu wa Serikali hadi Machi, imetumia **TZS 9.555 bilioni** sawa na asilimia **90** ya makadirio ya kutumia **TZS 10.649 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu Kuu zifuatazo:-

***PF0501 – Programu Kuu ya Usimamizi wa Hazina***

43. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2025, Programu hii imetumia **TZS 0.370 bilioni** sawa na asilimia **61** ya makadirio ya kutumia **TZS 0.611 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu Kuu hii imejumuisha Programu Ndogo nne nazo ni:

i. Programu ya Ufuatiliaji wa Mapato ya Serikali Yasiyokuwa ya Kodi. Programu hii hadi Machi imetumia **TZS 0.007 bilioni** sawa na asilimia **19** ya makadirio ya kutumia **TZS 0.039 bilioni;**

ii. Programu ya Kusimamia Ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali Machi 2025 imetumia **TZS 0.116 bilioni** sawa na asilimia **91** ya makadirio ya **TZS 0.127 bilioni;**

iii. Programu ya Usimamizi wa Matumizi ya Serikali, hadi Machi imetumia **TZS 0.138 bilioni** sawa na asilimia **40** ya makadirio ya kutumia **TZS 0.345 bilioni**; na

iv. Programu ya Usimamizi wa Deni la Taifa: Programu hii imetumia **TZS 0.109 bilioni** sawa na asilimia **109** ya makadirio ya **TZS 0.101 bilioni.**

44. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya ufuatiliaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi katika Wizara/ Taasisi mbalimbali za Serikali ili kujua changamoto na mafanikio hali iyo imepelekea ongezeko la asilimia 21 na kufikia **TZS 155.168 bilioni** kutoka **TZS 121.836 bilioni** kwa mwaka 2023/2024;

ii. Kusimamia na kuratibu maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa Viwango vya Uandaaji Hesabu kwa mfumo wa "IPSAS Accrual" kwa kuwajengea uwezo timu ya usimamizi wa mradi, wahasibu, watunza mali pamoja na kutoa miongozo ya uandaaji wa salio la kuanzia (opening balance);

iii. Kuratibu malipo ya mikopo kutoka Benki (PBZ, NBC, CRDB), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Hati Fungani za Serikali zilizoiva;

iv. Kutoa mikopo ya maafa kwa wafanyakazi 439 kutoka katika taasisi mbalimbali za Serikali;

v. Kuratibu upatikanaji wa Hati Fungani Yenye Kuzingatia Misingi ya Shariah (SUKUK); na

vi. Kufanya uhakiki wa wastaafu wanaopokelea pencheni Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ambapo wastaafu 13,250 wamehakikiwa sawa na asilimia 88 ya makadirio yaliyowekwa ambayo yalikuwa ni 15,066.

***PF0502 – Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali***

45. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi Programu hii imetumia **TZS 9.185 bilioni** sawa na asilimia **91** ya makadirio ya **TZS 10.038 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu kuu hii imejumuisha Program Ndogo zifuatazo:-

i. Programu ya Utawala na Uendeshaji Unguja. Hadi Machi Programu hii imetumia **TZS 6.79 bilioni** sawa na asilimia **89** ya makadirio ya kutumia **TZS 7.612 bilion**i kwa kipindi cha tathmini;

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango na Sera. Programu hii imetumi**a TZS 0.023 bilioni** sawa na asilimia **29** ya makadirio ya kutumia **TZS 0.079 bilion**i kwa kipindi cha tathmini; na

iii. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Pemba, hadi Machi 2025, imetumia **TZS 2.372 bilioni** sawa na asilimia **101** ya makadirio ya kutumia **TZS 2.347 bilion**i kwa kipindi cha tathmini.

**46. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Malipo ya wafanyakazi 12 waliokwenda likizo ya kawaida pamoja na kutayarisha stahiki za wafanyakazi wawili ambao wamestaafu;

ii. Kuandaa tovuti ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na kwa sasa ipo katika hatua za mwisho za kufanyiwa mapitio;

iii. Kuandaa mpango mkakati wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; na

iv. Usimamizi wa mapato, uratibu wa shughuli za Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Pemba na kuwajengea uwezo watendaji 9.

**Fungu F06 (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali)**

**47. Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2025, Ofisi imetumia **TZS 3.769 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya kutumia **TZS 4.820 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Matumizi hayo yamejumuisha Programu kuu mbili ambazo ni: -

***PF0601- Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini***

48. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2025, Programu hii imetumia **TZS 0.160 bilioni** sawa na asilimia **21** ya makadirio ya kutumia **TZS 0.753 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha Programu Ndogo tatu (3) ambazo ni:-

    i. Programu Ndogo Usimamizi wa Kamati za Ukaguzi na Taarifa Jumuishi za Ukaguzi wa Ndani; hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 0.033 bilioni** sawa na asilimia **28** ya makadirio ya **TZS 0.117 bilioni** kwa kipindi cha tathmini;

    ii. Programu Ndogo ya Uchunguzi wa Ubadhirifu na Vihatarishi; hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 0.083 bilioni** sawa na asilimia **23** ya makadirio ya **TZS 0.361 bilioni** kwa kipindi cha tathmini; na

    iii. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uthibitisho wa Ubora, hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 0.045 bilioni** sawa na asilimia **16** ya makadirio ya **TZS 0.274 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

49. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

    i. Kufanya ukaguzi maalum kwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) kwa kukagua mapato na matumizi, Mikataba, Ufuataji wa Sheria na Miongozo pamoja na Utafiti wa Kiufundi (Technical aspects);

    ii. Kutoa mafunzo ya Ukaguzi wa Mifumo (CISA) kwa wakaguzi wa ndani 34 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuikagua mifumo inayotumika katika Taasisi za Umma; na

    iii. Kuandaa muongozo wa usimamizi wa viashiria hatarishi unaotarajiwa kutumika katika Taasisi zote za Umma na kutoa

mafunzo ya ukaguzi wa Viashiria Hatarishi kwa wakaguzi wakuu wa ndani wa Taasisi za Umma kwa lengo la kuwawezesha kugundua na kuzuia viashiria vinavyoweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo katika Taasisi za Umma.

***PF0602 - Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji***

50. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2025, Programu hii imetumia **TZS 3.609 bilioni** sawa na asilimia **89** ya makadirio ya kutumia **TZS 4.067 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni:

    i. Program Ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango, Mafunzo na Utafiti, hadi Machi 2025, imetumia **TZS 2.901 bilioni** sawa na asilimia **90** ya makadirio ya kutumia **TZS 3.223 bilioni** ya kipindi cha tathmini; na

    ii. Program Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba, hadi Machi 2025, imetumia **TZS 0.707bilioni** sawa na asilimia **84** ya makadirio ya **TZS 0.844 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

51. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

    i. Kutayarisha Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT Policy) kwa lengo la kutoa muongozo wa kusimamia utekelezaji wa operesheni za TEHAMA, pamoja na Sera ya Usalama wa TEHAMA (ICT Security Policy) kwa lengo la kuhakikisha Ulinzi na Usalama wa taarifa na operesheni za Ofisi;

    ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali katika kuboresha ufanisi wa Mfumo wa ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi (GARI-ITS)", ambapo watendaji wanne (4) wa mfumo wamepatiwa mafunzo hayo kutoka kwa watengezaji wa mfumo na Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali-Tanzania Bara; na

iii. Kuandaa vikao vya Kamati ya Ukaguzi ambavyo vimejadili taarifa ya ukaguzi wa ndani ya robo ya nne ya mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Taarifa ya ukaguzi wa ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**Fungu F07 (Ofisi ya Msajili wa Hazina)**

52. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai-Machi 2024/2025, Ofisi imetumia **TZS 2.562 bilioni** sawa na asilimia **65** ya makadirio ya kutumia **TZS 3.942 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Matumizi hayo yamejumuisha Programu kuu mbili ambazo ni:-

***PF0701 Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma***

53. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu imetumia **TZS 0.992 bilioni** sawa na asilimia **40** ya makadirio ya **TZS 2.473 bilioni** ya kipindi cha tathmini Programu hii imejumuisha Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni:-

i. Program Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma, hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 0.861 bilioni** sawa na asilimia **43** ya makadirio ya **TZS 1.982 bilioni** kwa kipindi cha tathmini; na

ii. Program Ndogo ya Usimamizi wa Mali za Umma, hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 0.131 bilioni** sawa na asilimia **27** ya makadirio ya **TZS 0.491 bilioni** kwa kipindi cha tathmini.

54. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025 Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuchambua taarifa za kifedha za Mashirika sita (6) yanayotumia mfumo wa "Accrual Basis" na kugundua uwepo wa vihatarishi vya kifedha kwa baadhi ya Mashirika. Aidha ripoti hiyo imejaribu kutoa hali halisi ya Utendaji wa Shirika kwa kipindi cha Miaka

Mitatu na kutolewa kwa ushauri wa namna bora ya kupambana na vihatarishi hivyo kwa miaka ijayo;

ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mashirika 6 ya Uwekezaji ili kubaini mafanikio na changamoto zinazoyakabili;

iii. Kuandaa Rasimu ya Muongozo wa Mkataba wa Utendaji kazi kwa Bodi ya Wakurugenzi na Menejmenti ya Mashirika ya Uwekezaji wa Umma, Mpango wa Tathmini ya Mkataba wa Utendaji kazi, Rasimu ya Mpango Mkakati wa Mashirika ya Uwekezaji ya Taasisi za Umma na Rasimu ya Sera ya Mashirika ya Uwekezaji wa Umma;

iv. Kukamilisha Muongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma;

v. Ofisi imeweza kufanikisha kutoa mafunzo juu ya mfumo wa usimamizi wa mali ZGAMIS kwa taasisi 52 za Serikali ili kujenga uwelewa kwa wasimamizi wa mali kwa ajili ya kuingiza taarifa kwa usahihi katika mfumo huo; na

vi. Ofisi imeendelea na utaratibu wa uanzishwaji wa Kitengo cha Usimamizi wa Mali za Serikali (AMU) katika taasisi za Umma zinazohitajika uwepo wa kitengo hicho ambapo zaidi ya taasisi 126 zimeorodheshwa na kuwasilishwa Utumishi wa Umma kuendelea na zoezi.

***PF0702 Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa shughuli za Ofisi ya Msajili Hazina***

55. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, program hii imetumia **TZS 1.569 bilioni** sawa na asilimia **107** ya makadirio ya **TZS 1.468 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni:-

i. Program Ndogo Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango, Mafunzo na Utafiti, hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 1.302 bilioni** sawa na asilimia **128** ya makadirio ya **TZS 1.018 bilioni** ya kipindi cha tathmini; na

ii. Program Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 0.267 bilioni** sawa na asilimia **59** ya makadirio ya **TZS 0.451 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

56. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Programu Ndogo hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuandaa rasimu tatu (3) za miongozo ya Usimamizi wa Mali za Serikali ambayo ni Muongozo wa mgawanyo wa mali, njia ya kushuka thamani na viwango kwa Taasisi za Umma, Muongozo kuhusu utaratibu na Uhakiki wa Mali za Umma na Muongozo wa Mpango wa ubadilishaji wa Mali za Umma wa mwaka;

ii. Kufanyika kwa ukaguzi wa vyombo vya moto, mitambo na mashine kwa Wizara (7) na Taasisi (23) za Serikali kwa upande wa Pemba ambapo jumla ya Mali 529 zilikaguliwa kwa kuangaliwa hali halisi ya mali hizo;

iii. Kusimamia maslahi ya watumishi, jumla ya wafanyakazi 37 wamepatiwa malipo ya mishahara na wafanyakazi 20 wamefanyiwa taratibu za malipo ya stahiki mbalimbali kama vile; malipo ya malimbikizo ya mshahara na posho kwa kufanya kazi mbalimbali;

iv. Kukagua Maghala ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda waliyokabidhiwa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Mali Asili na Mifugo kwa ajili ya kuyafanyia ukarabati na kuweza kuyatumia kwa kuhifadhia chakula. Hatua za kufanyiwa ukarabati zinaendelea kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo; na

v. Kukagua majengo tisa (9) na sehemu za wazi mbili zilizokodishwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Pemba, ukaguzi huo ulibaini kuwa kuna baadhi ya Majengo hali yake sio nzuri na yanahitaji ukarabati. Ofisi imeamua kufanya mchakato wa kuyatangaza majengo hayo kwa wazabuni wa ndani ili kuyafanyia ukarabati.

## E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2024/2025

***Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi (BIG – Z)***

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi ina lengo la kuimarisha miundombinu, haiba ya Zanzibar na kukuza Maendeleo ya kiuchumi katika utoaji wa huduma, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa Miji. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii ilikadiriwa kutumia **TZS 32 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

58. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufika Machi 2025, Programu imetumia **TZS 14.683 bilioni** sawa na asilimia **73** ya makadirio ya **TZS 20 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

    i. Ujenzi wa mitaro wa eneo la Sebleni na Wandarasi hadi bwawa la vijibwa umekamilika, Ujenzi wa mitaro unaendelea katika maeneo ya barabara ya Sogea Denja, Magomeni Jitini (Shimo la nguruwe) mtaro wa pembezoni mwa barabara ya Kwamchina mwanzo hadi Magereza (Jang'ombe green corridor), Mtaro wa barabara ya Magomeni-KwaNajim hadi uwanja wa Wandarasi unaoungana na bwawa la Vijibwa na Mtaro wa Kwa Boko – Magazeti unaendelea na hadi kufikia Machi, ujenzi huu umefikia asilimia 59 kwa mradi;

    ii. Ujenzi wa Barabara ya Jang'ombe pamoja na kuanza ujenzi wa Barabara ya Sogea – Denja na Barabara ya Magazeti – Kwa Boko. Hadi kufikia Machi, ujenzi huu umefikia asilimia 42;

    iii. Ununuzi wa vifaa vya usafi (Gari 2 za kubebea taka, Makontena 10 ya kubebea taka pamoja na vikapu 20 vya kubebea taka) kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa Unguja na Pemba umefanyika;

iv. Kukamilika na kukabidhiwa kwa ripoti za pembuzi yakinifu, usanifu wa michoro na kuandaa nyaraka za zabuni kwa miradi ya mji salama kwa watembea kwa miguu Mji Mkongwe na kuendeleza eneo la Michenzani; kuimarisha miji ya Pemba; ujenzi wa maeneo ya utalii ya Nungwi, Chwaka na Makunduchi pamoja ujenzi wa vituo vya kukusanyia taka.

***Program ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali***

**59. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya kazi ili kuimarisha ufanisi katika kutoa huduma stahiki kwa wananchi. Kwa mwaka 2024/25 Programu imepangiwa **TZS 113.98 bilioni** kutoka Serikalini ambazo fedha hizo zimejumuisha fedha za Ujenzi wa Mji wa Serikali na Ukamilishaji wa Ofisi za Serikali. hadi kufika Machi, 2025 **TZS 13.658 bilioni** zimetumika kwa ajili ya ukamilishaji wa Ofisi za Serikali sawa na asilimia **38** ya makadirio ya **TZS 35.890 bilioni,** fedha zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi umefikia asilimia 95;

ii. Ujenzi wa Ofisi ya Mufti Zanzibar umekamilika;

iii. Ujenzi wa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali umefikia asilimia **85;**

iv. Ujenzi wa Ofisi ya Shirika la Magazeti umefikia asilimia **65;**

v. Kuboresha Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka umekamilika;

vi. Ujenzi wa Ofisi ya Nyaraka asilimia **36;** na

vii. Ujenzi wa Nyumba za Mombasa umekamilika.

**60. Mheshimiwa Spika,** Kuhusu wa ujenzi wa Mji wa Serikali, kampuni saba zimeonesha nia na kufanya mazungumzo na Serikali kuhusu ujenzi huo, hata hivyo bado Serikali inaendelea kupitia nyaraka zao kwa lengo la kufanya maamuzi.

***Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP – VI)***

61. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Programu imepangiwa **TZS 0.400 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 4.458 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo hadi kufikia Machi 2025 Programu imetumia **TZS 2.04 bilioni** sawa na asilimia **56** ya makadirio ya **TZS 3.643 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekelezwa shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha na kuanzisha mifumo inayohusiana na usimamizi wa kodi, ukaguzi pamoja na usimamizi wa mpango wa bajeti, hadi kufika Machi, mifumo miwili imekamilika;

ii. Kufanya mapitio na kutoa miongozo inayohusiana na sheria mbali mbali za mapato, matumizi, udhibiti na ukaguzi; hadi kufikia Machi, mradi huu umefikia asilimia 60 kwa kukamilisha baadhi ya shughuli zikiwemo Mpango Mkakati wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri elekezi wa kodi na Mwongozo wa Viashiria hatarishi (Risk management Framework) ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango;

iii. Watumishi 219 sawa na asilimia 60 wamejengewa uwezo kuhusiana na mipango, bajeti, uthibiti, ukaguzi na wasimamizi wa fedha za umma; na

iv. Kushiriki ziara za kujifunza ili kuongeza uwelewa juu ya usimamizi wa fedha za umma na udhibiti.

***Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM)***

62. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la mradi huu ni kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili. Kwa mwaka 2024/25, Mradi huu umepangiwa kutumia **TZS 1.065 bilioni** hadi kufika Machi, 2025 **TZS 0.329 bilioni** zimetumika sawa na asilimia **65** ya makadirio ya **TZS 0.500 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika

kwa kuandaa Sheria na Miongozo ya Madini, Sheria ya Usimamizi wa Mapato yatokanayo na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na uendeshaji wa mradi.

***Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP)***

63. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) inaendelea na Utekelezaji wa Programu ya Uimarishaji Takwimu Awamu ya Pili (Tanzania Statistical Master Plan II") kwa lengo la kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar ili kuwezesha upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida (routine data) kwa wakati. Mpango huu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umekadiriwa kutumia **TZS 8.66 bilioni.** Hadi kufika Machi 2025, Mpango umetumia **TZS 3.68 bilioni** sawa na asilimia **42** ya makadirio **TZS 6.77 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Utafiti wa Ajira na Mapato kwa mwaka 2023/24, Ofisi imewasilisha matokeo ya Utafiti wa Uajiri na Mapato wa mwaka 2022/2023 ambapo jumla ya taasisi 2,210 zilihojiwa Unguja na Pemba;

ii. Utafiti wa Watu wenye uwezo wa kufanya kazi mwaka 2024 (ILFS), Zoezi la ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi 2024 limekamilika kazi inayoendelea kwa sasa ni uchambuzi wa taarifa ambapo ripoti yake inategemewa kutolewa Juni 2025;

iii. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania wa mwaka 2024/2025 Ofisi inaendelea kazi ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya ambayo ilianza Januari, 2025;

iv. Sensa ya uzalishaji viwandani ya mwaka 2023 (CIP, 2023) Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inaendelea na matayarisho ya kufanya Sensa ya Uzalishaji Viwandani ambapo hadi sasa kazi inayofanyika ni ukusanyaji wa taarifa za viwanda;

v. Programu ya Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia, Ofisi imeendelea na kazi za ukusanyaji wa taarifa pamoja na kuandaa ripoti ya Takwimu za Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto ambayo huwasilishwa kwa wadau kupitia vyombo vya habari kila mwezi; na

vi. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania wa Mwaka 2024/2025, Ofisi inaendelea kazi ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya ambayo ilianza Januari, 2025.

***Programu ya Kurasimisha Ardhi na Biashara Zanzibar***

**64. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuinua hali za wananchi kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili ziweze kutumika katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii ilikadiriwa kutumia **TZS 3.00 bilioni.** Hadi kufikia Machi 2025, **TZS 1.45 bilioni** zimetumika sawa na asilimia **49** ya makadirio ya **TZS 2.94 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Viwanja **555** vimepimwa (Unguja 397, Pemba 158) na hati **645** zimetolewa kwa Wananchi (Unguja 491, Pemba 154). Aidha, Vipindi viwili (2) vya TV kupitia ZBC TV, viwili (2) kupitia ZBC Redio na kimoja (1) kupitia Redio Mtegani (Redio Jamii) vimefanyika kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kusajili Ardhi zao ili kuepuka migogoro inayoweza kutokea katika umiliki wa Ardhi;

ii. Ziara za ufuatiliaji zilifanyika katika Kituo cha Urasimishaji Ardhi cha Makunduchi ambapo ujenzi umekamilika, pamoja na kukagua makabati ya kielektroniki ya kuhifadhi taarifa za Ardhi katika Masjala ya Ardhi Mwanakwerekwe ambayo ujenzi wake umekamilika. Pia, ziara hizo zilihusisha ukaguzi wa maeneo yaliyopimwa yakiwemo Maungani na Makunduchi (Unguja) na Makangale (Pemba), pamoja na eneo litakalojengwa Kituo cha

Masjala ya Ardhi katika Wilaya ya Chake Chake Pemba. Vilevile, vifaa vya upimaji Ardhi (plotta, printa, kompyuta, na GPS) vilivyonunuliwa na Mradi vilikaguliwa ili kubaini utendaji wake.

iii. Wajasiriamali na Wafanyabiashara **810** waliopatiwa mafunzo, wametembelewa katika Wilaya ya Kusini, Wilaya ya Mjini kwa Unguja, Micheweni na Chake Chake kwa Pemba kujuwa maendeleo katika uendeshaji wa shughuli zao za kibiashara.

iv. Wajasiriamali na Wafanyabiashara wadogo wadogo 1,020 (Wete 250, Kati 200, Mjini Magharib 250, Kaskazini Unguja 200, Magharibi "B" 50, Kusini 70) wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa biashara, ikiwemo jinsi ya kuweka kumbukumbu, mbinu za uendeshaji wa biashara, fursa za mikopo katika benki na Taasisi za uwezeshaji, pamoja na umuhimu wa kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii kama ZSSF na usajili wa biashara zao kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) ambapo kati ya hao wafanya biashara 409 walisajili biashara zao.

***Mradi wa Mapitio, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa (ZADEP, ZDV 2050, SDGs na African Agenda)***

65. **Mheshimiwa Spika,** Mradi una lengo la kuimarisha Uratibu, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, umepangiwa kutumia kiasi cha **TZS 2.28 bilioni** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi **TZS 0.44 bilioni** zilitumika sawa na asilimia **22** ya makadirio **TZS 2.02 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kushiriki katika Mikutano ambapo ripoti ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa mwaka 2023 iliyounganishwa na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na iliwasilishwa Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa;

ii. Kufanya mapitio ya muda wa kati wa utekelezaji wa mpango wa maendeleo Zanzibar( ZADEP 2021-26), Kazi hii imefanyika na itawasilishwa katika kikao cha Tume ya Mipango kama ulivyo utaratibu;

iii. Kufanya mafunzo ya muda mfupi ya ufuatiliaji na tathmini kwa Maafisa saba kutoka MDAs, LGAs; na

iv. Kufanya Mapitio na mafunzo ya mfumo wa kidigitali wa Mipango ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo (MDAs, LGAs).

## F. UTEKELEZAJI WA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI -MACHI, 2024/2025

### *i. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)*

66. **Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Julai - Machi 2025, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imekusanya jumla ya **TZS 667.78 bilioni** sawa na asilimia **102** ya makadirio ya **657.815 billioni** katika kipindi cha tathmini. Ongezeko la mapato hayo limesababishwa na mikakati ifuatayo:-

i. Kuimarika kwa ufuatiliaji na usimamizi wa walipakodi, ikiwemo matumizi ya mifumo ya kisasa ya TEHAMA inayowezesha ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za biashara na ulipaji kodi.

ii. Uhamasishaji wa walipakodi kuhusu wajibu wa kulipa kodi, kupitia kampeni za elimu kwa umma na ushirikiano na wadau wa sekta binafsi.

iii. Upanuzi wa wigo wa walipakodi kwa kusajili vyanzo vipya vya mapato na kuwafikia wafanyabiashara waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa ulipaji kodi.

iv. Ukusanyaji wa madeni ya kodi kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisheria na kiutawala.

v. Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi hasa katika sekta za biashara, huduma na utalii, ambazo zimechangia kuongeza kiwango cha mapato.

vi. Uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane.

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) hadi kufikia Machi 2025, imetumia **TZS 22.642 bilioni** sawa na asilimia **97** ya makadirio ya **TZS 23.383 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Kati ya fedha hizo **TZS 21.017 bilioni** zilitokana na ruzuku kutoka Serikalini na **TZS 1.63 bilioni** zimetokana na makusanyo ya ndani ya **ZRA.**

### *ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*

68. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar imefanikiwa kukusanya kiasi cha **TZS 473.318 bilioni** ya makadirio ya kukusanya **TZS 600.082 bilioni** sawa na asilimia **79** ya lengo la kipindi cha tathmini. Mafanikio haya yametokana na mikakati ifuatayo:-

i. Uboreshaji wa mifumo ya Forodha na kodi za ndani (Enhancement TANCIS na Upgraded E-Filing System), ambapo mifumo hii humrahisishia mfanyabiashara kujikadiria kodi mwenyewe na kutengeneza Control Number ya malipo;

ii. Ufunguzi wa vituo viwili (Tax Centres) vilivyopo Kiwengwa na Paje na kuimarisha mifumo ya Kielektroniki na;

iii. Kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi.

### *iii. Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)*

69. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA), ilikadiriwa kukusanya **TZS 0.989 bilioni** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato ikiwemo usajili wa watoa huduma, ada ya mafunzo ya mpango wa manunuzi, ada ya nyaraka za zabuni na matangazo ya zabuni. Hadi Machi 2024, Mamlaka imekusanya **TZS 0.446 bilioni** sawa na asilimia **62** ya makadirio **TZS 0.718 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

70. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, hadi Machi 2025, Mamlaka imetumia **TZS 1.566 bilioni** sawa na asilimia **60** ya kupokea ruzuku ya **TZS 2.617 bilioni** kwa kipindi cha tathmini kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

   i. Kukagua Taasisi nunuzi 37 Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha usimamiaji na utumiaji wa Sheria unatekelezwa ipasavyo;

   ii. Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo ya mfumo wa ununuzi wa mtandao (e-Proz) kwa Bodi ya Zabuni na watendaji wa ununuzi kwa Taasisi nunuzi kwa upande wa Unguja na Pemba;

   iii. Mamlaka imesajili watoa huduma 630 kwa kupitia mfumo wa ununuzi wa mtandao (e-Proz);

   iv. Kutayarisha nyaraka sanifu za huduma ya Mshauri elekezi (Standard Bidding Document for Individual Consultancy);

   v. Kukamilisha Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 2 ya Mwaka 2025;

### *iv. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)*

71. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko umekusanya mapato **TZS 199.08 billioni** sawa na asilimia 81 ya makadirio ya **TZS 246.34 bilioni** kutoka katika vyanzo vikuu

viwili, ambavyo (michango ya wanachama **TZS 114.13 bilioni** na mapato ya uwekezaji **TZS 84.95 bilioni**).

72. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2025 Mfuko umetumia **TZS 328.80 bilioni** sawa na asilimia **92** ya makadirio ya **TZS 351.4 bilioni** katika kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Mfuko umesajili waajiri 245 sawa na asilimia 85 ya makisio ya kuwasajili waajiri 286. Hadi sasa Mfuko umekuwa na Waajiri waliosajiliwa kufikia 3,327;

ii. Mfuko umesajili waajiriwa 11,655 sawa na asilimia 53 ya makisio ya kuwasajili waajiriwa 21,767. Wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi Machi 2025, wamefikia 153,351 kwa Mfuko wa lazima;

iii. Waajiri 1,085 walitarajiwa kufanyiwa ukaguzi. Waajiri 1,765 wamekaguliwa, kati ya hao waajiri 750 walikaguliwa kwa ufuatiliaji (Follow-up), waajiri 702 walikaguliwa kwa ukaguzi wa kawaida (Routine) na waajiri 313 walikaguliwa katika zoezi la ukaguzi la waajiri wapya (Survey Inspection);

iv. Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar unaendelea kukusanya michango ya asilimia moja (1%) kutoka kwa waajiri kuhusiana na Fao la kuumia kazini;

v. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Majengo 14 yanaendelea kujengwa na utekelezaji umefikia asilimia 85 na mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi;

vi. Ujenzi wa mradi wa viwanja vya Michezo na Biashara Mbweni; Mradi umekamilika na mkandarasi amemalizia kufanya marekebisho madogo madogo; na

vii. Kuendelea na Ujenzi wa Soko la Mombasa ambapo kazi za kupiga plasta ya sehemu ya chini na ujenga wa vizimba zinaendelea.

Mradi umefikia asilimia 55 na unatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### *v. Shirika la Bima (ZIC)*

73. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Shirika yanatokana na vianzio vyake vya mauzo ya Bima pamoja na faida zinazotokana na Uwekezaji, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2025, Shirika limefanikiwa kukusanya **TZS 82.3 bilioni** ya mauzo ya Bima pamoja na mapato yatokanayo na uwekezaji ambayo ni sawa na asilimia **142** ya makadirio ya kukusanya **TZS 57.8 bilioni** katika kipindi cha tathmini. Ongezeko hilo la asilimia **42** limechangiwa na mapato yanayotokana na uanzishwaji wa Bima ya Lazima "Inbound Travelling Insurance" kwa wageni wanaoingia Zanzibar.

74. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi 2025, Shirika limetumia jumla ya **TZS 16.7 bilioni** ambapo **TZS 6.8 bilioni** zimetumika kulipa madai mbalimbali ya wateja waliopata ajali na kutimiza matakwa ya Sheria za bima, **TZS 2.8 bilioni** zimetumika kulipa ujira kwa Mawakala na Madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika na **TZS 7.2 bilioni** kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa ofisi.

### *vi. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)*

75. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, PBZ imeendelea kukuza mapato yake halisi na kufikia **TZS 161.534 bilioni** ikiwa ni sawa na asilimia 93 ukilinganisha na mapato yaliokadiriwa ya **TZS 173.439 bilioni.** Halikadhalika mapato hayo yaliongezeka kwa asilimia **23** ukilinganisha na mapato ya **TZS 131.615 bilioni** katika kipindi kama hicho cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Ongezeko la Mapato kwa kiwango kikubwa kimesababishwa na kuongezeka faida za mikopo, faida ya Benki ya kiislam, huduma za kieletroniki (ATMs, MOBILE BANKING, PBZ APP na INTERNET BANK) kwa kipindi hicho.

76. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, PBZ imetumia **TZS 88.73 bilioni** ukilinganisha na makadirio ya **TZS 100.67 bilioni** sawa na asilimia 88 kwa kipindi cha tathmini. Aidha, Benki imeweza kufikia lengo la kupata faida kwa asilimia **100** katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025 kutoka kiwango kilichokadiriwa cha **TZS 72.768 bilioni** na kufikia **TZS 72.809 bilioni.**

77. **Mheshimiwa Spika,** PBZ ni miongoni mwa walipakodi wakubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA). Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 mpaka Machi 2025), imefanikiwa kulipa kodi ya **TZS 34 billioni** ikiwa ongezeko la ulipaji wa asilimia **14** ukilinganisha na kiwango cha **TZS 30 billioni** iliyolipwa katika kipindi cha Julai 2023 mpaka Machi 2024.

### *vii. Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT)*

**Mapato**

78. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi cha Julai-Machi 2024/2025, kwa upande wa mapato ya ruzuku, Taasisi imepokea **TZS 0.913 bilioni** kutoka Serikalini sawa na asilimia **73** ya makisio ya **TZS 1.241 bilioni,** ambapo (TZS 0.625 bilioni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 0.259 bilioni** kwa ajili ya mishahara). Kwa upande wa mapato ya ndani, Taasisi imekusanya **TZS 0.29 bilioni** sawa na asilimia 38 ya makadirio ya **TZS 0.76 bilioni.** Upungufu wa makusanyo hayo umetokana na kuchelewa kufanya mafunzo kwa wanachama na wadau wengine, hata mafunzo hayo yamefanyika katika mwezi Mei 2025. Mapato yaliyokusanywa yametokana na ada ya usajili wa wanachama, ada ya mwaka ya wanachama (subscription fees), ada ya leseni kwa kampuni zinazofanya kazi (Practicing Firms) za kiuhasibu, ukaguzi na kodi, kuendesha mafunzo maalum kwa wafanyakazi wapya wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali na mafunzo ya muda mfupi kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Kamisheni ya Ardhi.

**79. Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa upande wa matumizi katika kipindi cha Julai-Machi 2024/2025, Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi imetumia **TZS 0.465 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni sawa na asilimia **38** ya makisio ya **TZS 1.24 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Fedha hizo zilitumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutayarisha Mpango wa Utekelezaji wa "Statement of Member Obligations (SMOs)" kwa ajili ya kujiunga na Shirikisho la Wahasibu Duniani (IFAC) ambapo kwa sasa umekamilika na tayari tumeanza kuitekeleza mpango huu unatusaidia kupata uanachama wa Shirikisho la Uhasibu;

ii. Kufanya Ufuatiliaji wa Wanachama Serikalini na Taasisi binafsi, hadi kufikia mwezi wa Machi 2025 jumla ya wanachama 615 wamesajiliwa katika ngazi tofauti na Kampuni 15 zimesajiliwa;

iii. Kuingia kwenye Makubaliano na TCU kwa ajili ya kuunganisha mifumo (intergration) ya usajili wa wanafunzi;

iv. Kutayarisha Mitaala ya Taaluma ya Kodi ambayo inategemewa kuanza June 2025;

v. Kutayarisha Muongozo wa Uthibitisho wa Ubora (Quality Assurance Manual) na Mpango Mkakakati wa Taasisi (Strategic Plan) tayari umekamilika na kuanza kutumika ili kuweza kufikia malengo tuliyojiwekea; na

vi. Kujenga uwelewa wa wanachama wa Taasisi katika kuilewa Sheria na Kanuni ya Taasisi, jumla ya wanachama 775 wamepatiwa uelewa.

## G. MASHIRIKIANO NA TAASISI NYENGINE

**80. Mheshimiwa Spika,** katika kufanya kazi zake na kufikia malengo iliyojiwekea, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imeendelea kushirikiana na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zikiwemo zifuatazo:

81. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imeshirikiana na Wizara ya Fedha katika upatikanaji wa rasilimali fedha za mikopo na misaada kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Wete, Tanzania Food System Resillience Program, Tanzania Maternal and child health Invenstment Project na Tanzania Social Action Fund na tayari imeanza kutekelezwa.

82. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi hii, tunaratibu uandaaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 kwa pamoja tokea hatua za awali ikiwemo kukusanya maoni kwa wananchi ili kupata maono ya Tanzania tuitakayo na kwa kuwasilisha Rasimu ya awali ya Dira ya Maendeleo ya 2050 kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

83. Ofisi kwa kushirikiana na Kitengo usimamizi wa Fedha Haramu (FIU) imeandaa rasimu ya marekebisho ya Sheria na Kanuni za Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu kwa lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

**MAFANIKIO**

84. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango katika Awamu ya Nane imepata mafanikio yafuatayo:-

i. Kuweza kukusanya kodi zaidi ya asilimia 100 ya kiwango kilichopangwa kwa Taasisi za kodi (TRA na ZRA);

ii. Serikali imeweza kununua gari zaidi ya 150 na kuweza kutatua changamoto ya usafiri kwa viongozi wa Serikali,kupunguza gharama na utofauti wa bei;

iii. Kuanzishwa kwa bima ya lazima kwa wageni wote wanaofika Zanzibar (Inbound Travel Insurance) ambayo inatoa kinga dhidi ya majanga na dharura pindi yakitokea ndani ya siku tisini na mbili (92) popote pale Zanzibar na Tanzania, aidha mapato ya Serikali yameongezeka;

iv. Serikali imetunga Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma Namba 2 ya Mwaka 2025 ambayo itarahisisha taratibu za ununuzi na kuongeza wigo wa aina za ununuzi;

v. Uratibu wa kifedha kwa ajili ya kufanikisha miradi ya kimkakati ikiwemo Mradi wa Usalama wa Maji kutoka ofisi ya GIZ Dar Es Salaam ambao umewezesha SMZ kupata Euro 25 Milioni kwa kutekeleza miundombinu ya maji kisiwani Pemba kwa maeneo ya Kangani, Ole, Pandani na Madenjani;

vi. Imefanikiwa kuongeza huduma za kifedha kwa kutunga Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha, kufungua matawi, vituo na Mawakala wa huduma za kibenki na bima pamoja na kuanzisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki;

vii. Serikali imefanikiwa kuanzisha njia nyingine ya kuhudumia miradi ya maendeleo kupitia Sukuk yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.15, ni ya muda wa miaka saba na inalenga kukusanya fedha kwa ajili ya kugharimia miradi ya kimkakati ya maendeleo ya Taifa. Kwa awamu ya kwanza, kiasi cha **TZS 381.385 bilioni** zimekusanywa sawa na asilimia **128**; na

viii. Kupitia ZSSF, Serikali imejenga Kituo cha Mabasi – kijangwani, Maegesho ya gari – Malindi na nyumba makaazi – Mbweni.

## CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

**85. Mheshimiwa Spika,** mbali na mafanikio yaliyopatikana Ofisi pia imekumbana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wake ikiwemo:-

i. Kuchelewa kukamilika kwa taratibu za miradi ikiwemo Big–Z, Mji wa serikali na ofisi zingine za serikali;

ii. Taasisi kushindwa kuwasilisha vielelezo vya kutosha vya Mradi na kupelekea kuchelewa kwa mradi kuanza;

iii. Utoaji wa Risiti kwa wafanyabiashara na wananchi kudai risiti bado ni tatizo;

iv. Ufinyu wa eneo la ofisi kwa watendaji wa Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango pamoja na baadhi ya taasisi zake.

86. **Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizoelezwa zimeendelea kutatuliwa kwa kupitia mikakati mbali ikiwemo:

i. Kwa kushirikiana na Benki ya Dunia Mradi wa Big Z kwa sasa utatekelezwa na Wizara mbili; Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili kurahisisha na kuharakisha utekelezaji wake;

ii. Ofisi imeanzisha Mfumo wa ZiPS (Zanzibar Intergrated Planning System) kwa lengo kurahisisha upatikanaji wa Taarifa za Miradi tokea awali;

iii. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuwaelimisha wananchi kudai risiti pamoja na kutoa adhabu kwa wafanyabiashara kwenye kukiuka suala la utoaji risiti; na

iv. Serikali inakamilisha hatua za kumtafuta mkandarasi/mbia kujenga wa Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka. Ujenzi unatarajiwa kuanza rasmi katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## H. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### Vipaumbele vya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango

87. **Mheshimiwa Spika,** bajeti hii imezingatia Dira ya Maendeleo 2050, Mpango Mkakati wa Maendeleo wa muda wa kati ZADEP, Ilani ya Chama cha Mapinduzi na maagizo yaliyotolewa katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi tarehe 11/11/2020. Vile vile, imezingatia mwenendo wa hali ya uchumi na mabadiliko ya teknolojia ya mifumo ya kielektroniki katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti upotevu wa mapato. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imejipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yakiwemo mapato ya ndani na mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

ii. Kuendelea kubuni vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo vikiwemo Hati Fungani ya SUKUK na mashirikiano na sekta binafsi kwa taratibu zikiwemo za EPC+F na PPP;

iii. Kukamilisha taratibu za kuanzisha Chuo cha Usimamizi wa Fedha Zanzibar (ZIFA) baada ya kutoka kuwa Skuli ya Biashara ya Chuo Cha Taifa cha Zanzibar (SUZA);

iv. Kukamilika na kusimamia utekelezaji wa Soko la Mitaji la Zanzibar (Zanzibar Securities Exchange);

v. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za viashiria vya uchumi, uwekezaji na maendeleo ya huduma za jamii;

vi. Kuandaa Mpango wa Maendeleo (ZADEP 2026 – 2031) pamoja na Mpango wa Utekelezaji, Mkakati wa Mawasiliano na Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini;

vii. Kuimarisha Mfumo Jumuishi wa Uandaaji na Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo Zanzibar (ZIPS) kwa kuunganisha na mifumo mengine inayohusiana na miradi ya maendeleo;

viii. Kufanya Mapitio ya Ajenda ya Utafiti (Zanzibar Research Agenda) ya Mwaka 2021/2026 na kuandaa Ajenda ya Utafiti kwa Mwaka 2026/2031;

ix. Kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Watu hapa Zanzibar, kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Rasilimali Watu pamoja na mfumo wa mafunzo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu na Vyuo vya Amali; na

x. Kuimarisha na kuongeza utekelezaji wa bajeti inayozingatia jinsia na usawa (Gender Responsive Budget) kwa Wizara na

Taasisi za Serikali kwa lengo la kuhakikisha fedha za umma zinapangwa na kutumika kwa mujibu wa mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii.

**Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango**

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango inakadiriwa kukusanya **TZS 6,527.599 bilioni,** makadirio hayo ni ongezeko la asilimia 33 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya **TZS 4,901.691 bilioni** yaliyopangwa kwa mwaka 2024/2025. Ongezeko hili linatarajiwa kutokana na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato, kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato na mikopo ya ndani kwa miradi ya maendeleo ikiwemo Hati Fungani ya Sukuk.

89. **Mheshimiwa Spika,** mapato hayo yamekadiriwa kukusanywa katika mafungu ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kama ifuatavyo: -

i. Fungu F01 limekadiriwa kukusanya TZS 3,518.630 bilioni;
ii. Fungu F04 limekadiriwa kukusanya TZS 0.180 bilioni;
iii. Fungu F05 limekadiriwa kukusanya TZS 2,980.289 bilioni; na
iv. Fungu F07 limekadiriwa kukusanya TZS 28.500 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa mapato hayo kwa kila chanzo unaonekana katika **kiambatanisho namba 3.**

**Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango.**

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango inakadiriwa kutumia **TZS 1,571.151 bilioni** makadirio hayo ni ongezeko la asilimia **38** ikilinganishwa na makadirio ya kutumia **TZS 1,133.21 bilioni** yaliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka jukumu la kusimamia Taasisi mpya na matumizi ya Serikali kuu. Uchambuzi wa Mafungu hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Fungu F01 limekadiriwa kutumia TZS 866.134 bilioni;
ii. Fungu F02 limekadiriwa kutumia TZS 641.350 bilioni;
iii. Fungu F03 limekadiriwa kutumia TZS 20.380 bilioni;
iv. Fungu F04 limekadiriwa kutumia TZS 11.607 bilioni;
v. Fungu F05 limekadiriwa kutumia TZS 17.589 bilioni;
vi. Fungu F06 limekadiriwa kutumia TZS 6.479 bilioni; na
vii. Fungu F07 limekadiriwa kutumia TZS 7.610 bilioni.

91. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa za matumizi naomba kuwasilisha uchambuzi wa matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa kila fungu kama ifuatavyo:-

**Matumizi kwa Fungu F01**

92. **Mheshimiwa Spika,** Fungu F01 limekadiriwa kutumia **TZS 866.134 bilioni** kati ya fedha hizo, **TZS 105.105 bilioni** ni mshahara (**TZS 99.904 bilioni** kwa ajili ya marekebisho ya mshahara na **TZS 5.201** mishahara ya Fungu F01), **TZS 37.877 bilioni** matumizi ya kawaida (kati ya fedha hizo **TZS 12.877 bilioni** Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **TZS 25 bilioni** ni Fedha za ununuzi wa gari kwa Taasisi zinazojitegemea), **TZS 36.877 bilioni** Ruzuku za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango (**TZS 30.16 bilioni** ZRA, **TZS 2.49 bilioni** ZIAAT, **TZS 0.951 bilioni** ZIFA na **TZS 3.27 bilioni** ZPPRA) na **TZS 686.274 bilioni** fedha za miradi ya maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu tatu (3) zifuatazo: -

i. Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma imekadiriwa kutumia **TZS 138.346 bilioni;**

ii. Programu ya Usimamizi wa Sera za Manunuzi na Masuala ya Sheria imekadiriwa **TZS 4.553 bilioni;**

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imekadiriwa **TZS 723.235 bilioni;**

**Matumizi kwa Fungu F02**

93. **Mheshimiwa Spika,** Fungu F02 limekadiriwa kutumia **TZS 641.350 bilioni**, kati ya fedha hizo, **TZS 3.013 bilioni** mishahara na **TZS 638.337 bilioni** matumizi ya kazi za kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Matumizi kwa Fungu F03**

94. **Mheshimiwa Spika,** Fungu F03 limekadiriwa kutumia **TZS 20.380 bilioni,** kati ya fedha hizo TZS 2.496 bilioni mshahara, **TZS 5.084 bilioni** matumizi ya kazi za kawaida na **TZS 12.800 bilioni** Matumizi ya kazi za Maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu tatu zifuatazo: -

i. Programu Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya watendakazi Programu imekadiriwa **TZS 14.786 bilioni;**

ii. Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti imekadiriwa kutumia **TZS 2.557 bilioni;** na

iii. Programu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango imekadiriwa kutumia **TZS 3.037 bilioni**.

**Matumizi kwa Fungu F04**

95. **Mheshimiwa Spika,** Fungu F04 limekadiriwa kutumia **TZS 11.607 bilioni** kati ya Fedha hizo, **TZS 2.486 bilioni** Mshahara, **TZS 2.203 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS 6.918 bilioni** kwa ajili ya Kazi za Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu mbili (2) zifuatazo: -

i. Programu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii **TZS 8.193 bilioni**; na

ii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali **TZS 3.414 bilioni**.

**Matumizi kwa Fungu F05**

96. **Mheshimiwa Spika,** Fungu F05 limekadiriwa kutumia **TZS 17.589 bilioni** kati ya Fedha hizo, **TZS 12.370 bilioni** mshahara, **TZS 0.650 bilioni** Ruzuku ya Kampuni ya Zanzibar Treasury Sukuk 1 Limited inayosimamiwa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, **TZS 3.545 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS 1.023 bilioni** kwa ajili ya Kazi za Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu Kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma **TZS 2.729 bilioni;** na

ii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali **TZS 14.860 bilioni.**

**Matumizi kwa Fungu F06**

97. **Mheshimiwa Spika,** Fungu F06 limekadiriwa kutumia **TZS 6.479 bilioni,** kati ya Fedha hizo, **TZS 4.481 bilioni** Mshahara na **TZS 1.998 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutumika kutekeleza Programu kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Huduma za Ukaguzi na Ushauri **TZS 1.201 bilioni;** na

ii. Programu ya Utawala na Uendeshaji **TZS 5.278 bilioni.**

**Matumizi kwa Fungu F07**

98. **Mheshimiwa Spika**, Fungu F07 limekadiriwa kutumia **TZS 7.610 bilioni**, kati ya fedha hizo, **TZS 1.113 bilioni** Mshahara na **TZS 6.497 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutumika kutekeleza Programu kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma **TZS 4.145 bilioni**; na

ii. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina **TZS 3.465 bilioni**.

99. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu zilizowasilishwa, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango itatekeleza Programu Ndogo Thelathini na Sita (36) ambazo uchambuzi wake unaonekana katika **Kiambatanisho namba 4.**

**Matumizi ya Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa Mwaka 2025/2026**

100. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imelenga kutekeleza Programu (5) na miradi (7) ya Maendeleo yenye thamani ya **TZS 707.017 billioni,** kati ya fedha hizo zimejumuishwa na fedha za Mpango wa Ulipaji wa Fidia za Miradi ya Maendeleo **TZS 210.399 bilioni** na fedha za ulipaji wa Madeni kwa Miradi ya Maendeleo **TZS 312.000 bilioni.** Mchanganuo wa miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ni kama ifuatavyo:-

***Programu ya Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISPDRM)***

101. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuandaa sheria na miongozo ya mapato yatokanayo na mafuta, gesi asilia na madini na kuwapatia mafunzo ya watendaji wa Serikali. Programu hii imekamilika na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 **TZS 0.50 bilioni** zilizokadiriwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa mradi kwa awamu inayofuata.

***Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z).***

102. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalenga kuimarisha hali ya maisha na kukuza maendeleo ya kiuchumi katika maeneo ya miji ya Zanzibar. Fedha za Programu hii ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii inakadiriwa kutumia **TZS 32.500 bilioni** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa.

***Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP IV).***

103. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalenga kuleta Mageuzi ya mifumo ya kifedha, miongozo ya kisheria ya usimamizi wa fedha na kujenga uwezo watendaji, fedha za Programu hii ni mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 inakadiriwa kutumia **TZS 4.750 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 4.400 bilioni** ni mkopo kutoka kwa Benki ya Dunia na **TZS 0.350 bilioni** kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

***Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali***

104. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalengo la kuweka mazingira bora ya kazi ili kuimarisha ufanisi katika kutoa huduma stahiki kwa wananchi. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii inakadiriwa kutumia kiasi cha **TZS 126.298 bilioni**. Kati ya fedha hizo **TZS 59.576 bilioni** ni fedha za mradi wa ukamilishaji wa Ofisi za Serikali na **TZS 66.722 bilioni** fedha za mradi wa Ujenzi wa Mji wa Serikali.

***Mradi wa Msaada wa kiufundi kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Uhamasishaji Utafutaji Rasilimali Fedha***

105. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalengo la kuratibu, kuhamisisha upatikanaji wa rasilimali fedha pamoja na kuwajengea uwezo watendaji kwa kuongeza ufanisi na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Fedha hizi ni msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 unakadiriwa kutumia **TZS 0.276 bilioni** Kati ya fedha hizo (**TZS 0.39 bilioni** mchango kutoka Ujerumani, **TZS 0.26 bilioni** mchango kutoka BADEA na **TZS 0.210 bilioni** mchango kutoka Benki ya Dunia).

***Mradi wa Mapitio, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, VISION 2050, SDGs 2030 na AFRICAN AGENDA 2063).***

**106. Mheshimiwa Spika,** Mradi una lengo la kuimarisha Uratibu, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi huu unakadiriwa kutumia **TZS 1.800 bilioni** kutoka Serikalini.

***Program ya Kuratibu Mpango wa Kurasimisha Ardhi na Biashara Zanzibar***

**107. Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuinua hali za wananchi kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili ziweze kutumika katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii inakadiriwa kutumia **TZS 4.500 bilioni** kutoka Serikalini.

***Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo***

**108. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuboresha uratibu na usimamizi wa mipango ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji mzuri na endelevu wa mikakati ya maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii inakadiriwa kutumia **TZS 5.500 bilioni** kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati***

**109. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuongeza uzalishaji na matumizi ya maarifa, teknolojia na bunifu ili kuongeza ushindani, mipango endelevu na kufanya maamuzi yanayotegemea ushahidi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi huu umekadiriwa kutumia **TZS 1.00 bilioni** kutoka Serikalini.

***Programu wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II)***

110. **Mheshimiwa Spika,** Mpango huu umelenga kuwezesha uzalishaji na usimamizi wa Takwimu, uimarishaji wa mifumo ya kitakwimu na miundombinu, Maendeleo ya Rasilimali Watu kwa Taasisi za Serikali kupitia Mfumo wa Takwimu Zanzibar ili kusaidia uimarishaji na upatikanaji wa Takwimu rasmi. Fedha hizi ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia, na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umekadiriwa kutumia **TZS 4.598 bilioni.**

***Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia***

111. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalengo la kuimarisha Takwimu za jinsia na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, mradi huu umekadiriwa **TZS 2.320 bilioni,** kati ya fedha hizo **TZS 2.00 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 0.320 bilioni** mchango kutoka kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN Women).

***Mradi wa Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IPSAS ACCRUAL)***

112. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalengo la kuboresha uwazi, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za umma kwa kuhakikisha taarifa za kifedha zinawasilisha hali halisi ya kifedha Serikalini. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umekadiriwa kutumia **TZS 1.023 bilioni** ambazo zinatoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango unaonekana katika **Kiambatanisho namba 5.**

## MWELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA 2025/2026

### Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

113. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Mamlaka ya Mapato imekadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 1,257.240 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 49 ya makadirio ya makusanyo ya mwaka 2024/2025 ambayo **TZS 845.979 bilioni.** Ongezeko hilo linatokana na mkakati wa Serikali wa Mapato yote yasiyokuwa ya kodi ya mawizara kukusanywa na Mamlaka na kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato. ZRA imekadiriwa kupokea ruzuku kutoka Serikalini ya **TZS 30.156 bilioni** kwa matumizi ya mishahara na uendeshaji wa Ofisi.

### Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

114. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar imekadiriwa kukusanya **TZS 825.769 bilioni** ni sawa na ongezeko la asilimia 38 ya makadirio ya makusanyo ya mwaka 2024/2025 ambayo yalikuwa ni **TZS 600.082 bilioni.**

### Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA) Mapato

115. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar, ZPPRA (iliyokuwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma), kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imekadiria kukusanya **TZS 1.175 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia **18** ya makadirio ya kukusanya ya **TZS 0.989 bilioni** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Mapato haya yatakusanywa kupitia vyanzo vyake vikiwemo: usajili wa watoa huduma, ada ya nyaraka za zabuni, matangazo ya zabuni na mafunzo.

**Matumizi**

116. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi Mamlaka, imekadiriwa **TZS 3.274 bilioni** ambayo ni ruzuku kutoka Serikalini kati ya hizo, **TZS 1.780 bilioni** kwa ajili ya ulipaji wa mishahara na **TZS 1.493 bilioni** kwa kutekeleza shughuli za ofisi zilizopangwa. Mamlaka itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi Umma na kutarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi kwa Taasisi nunuzi (60) na uchunguzi wa ununuzi kwa Taasisi nunuzi (8) pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba kwa Taasisi (15); na

ii. Kufanya mafunzo ya Sheria, kanuni na miongozo ya Ununuzi wa Umma kwa maafisa manunuzi, Maafisa Masuuli na Bodi ya Zabuni na mafunzo ya Nyaraka Sanifu za Ununuzi wa Umma kwa Watoa huduma.

**Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)**

**Mapato**

117. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko unatarajia kukusanya **TZS 360.50 billioni** kutoka katika vyanzo vikuu viwili ambavyo ni michango ya wanachama na mapato ya uwekezaji na mapato mengine, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mfuko unakadiria kukusanya **TZS 206.74 bilioni** kutokana na michango ya wanachama na **TZS 153.76 bilioni** kama mapato ya uwekezaji na mapato mengine.

**Matumizi**

118. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko unatarajia kufanya malipo ya mafao, usimamizi wa miradi na uwekezaji na gharama za uendeshaji kwa kiasi cha **TZS 360.50 billioni** kwa matumizi yake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kati ya hizo **TZS 17.34 billioni** kwa ajili ya gharama za uendeshaji, **TZS 117.03 billioni** kwa ajili ya Mafao na **TZS 226.13 billioni** kwa ajili ya usimamizi wa miradi na uwekezaji.

119. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na utekelezaji wa majukumu ya kawaida, Mfuko pia umepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuendelea kufanya uwekezaji wa fedha kwa kipindi cha muda mfupi na muda mrefu katika hatifungani, hatifungate, uwekezaji katika mabenki na kuendelea kutoa mikopo kwa Serikali, mashirika, taasisi na kampuni binafsi yenye tija katika Mfuko; na

ii. Kuanzisha rasmi utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa kuzingatia misingi ya sharia.

**Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

120. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Benki ya Watu wa Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yanakadiriwa kuongezeka kwa **asilimia 38** kutoka **TZS 201.4 bilioni** na kufikia **TZS 277.2 bilioni.** Ongezeko hilo litatokana na ongezeko la mapato ya riba yanayotokana na kuongeza kiwango cha utoaji wa mikopo kwa Benki ya Kawaida, matarajio ya kufungua matawi mapya katika mikoa ya Arusha, Tanga na Ubungo katika Mkoa wa Dar es salaam. Vile vile, faida itokanayo na uwezeshaji kupitia sharia na mapato yatakayotokana na uhamasishaji wa kutumia huduma za kieloktroniki kama vile huduma za mawakala, mashine za ATM, huduma za PBZ App, utumiaji wa kadi za VISA, internet banking na huduma za mobile banking.

121. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia **43** kutoka **TZS 109. 3 bilioni** na kufikia **TZS 156.7 bilioni,** Ongezeko la matumizi yatatokana na gharama mbalimbali za matawi mapya na vituo vipya vya kutolea huduma pamoja na matumizi ya kuboresha mifumo mbalimbali ya kibenki.

***Miradi inayotarajiwa kutekelezwa na PBZ kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026***

**122. Mheshimiwa Spika,** PBZ inaendelea na ujenzi wa matawi katika mikoa ya Arusha, Tanga na Ubungo katika mkoa wa Dar es salaam pamoja na kuendelea na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma (service centres) katika maeneo ya Pemba (ZSTC Madungu na Konde), na inatarajia kufanya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma kwa Unguja (Kiwengwa na Kwanyanya Market) na Tunduma.

**123. Mheshimiwa Spika,** PBZ kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kuweka mashine za kutolea fedha ATM katika maeneo ya KVZ-Mtoni, Jumbi, Dunga, Kizimkazi/Jambiani, Wingwi Mapofu na Mkokotoni pamoja na kuboresha miundombinu ya TEHAMA kwa kununua switchi yake (Financial Switch) ambayo itarahisisha na kuiongezea mapato benki kwenye huduma za mashine za kutolea fedha (ATM).

**124. Mheshimiwa Spika**, Kutokana na maelekezo ya mamlaka ya Mkoa wa Dar es salaam kufanya biashara katika eneo la Kariakoo kwa masaa 24, PBZ imeshaanza zoezi hilo kwa tawi lake la Kariakoo na inategemea kuimarisha miundo mbinu hitajika ili iwe endelevu.

**Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC)**

**Mapato**

**125. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima kwa Mwaka Fedha 2025/26 linatarajia kukusanya **TZS 57.3 bilioni** kutoka katika vianzio vyake vya mapato kwa kutekeleza mikakati ifuatayo: -

i. Kuendelea kutoa taaluma na kujitangaza kwa Wananchi waliopo mjini na vijijini na Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja wapya na mapato ya Shirika; na

ii. Shirika kuendelea kuzidisha mashirikiano kwa mawakala na madalali wake wanaofanya baishara ya kuuza Bima kwa niaba ya Shirika; vilevile kuendelea kushirikiana kikamilifu na mabenki mbalimbali katika mfumo wa "Bancassurance" kwa lengo la kuongeza mapato yake.

**126. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 limekadiriwa kutumia **TZS 40.1 bilioni** ikijumuisha matumizi yafuatayo:

i. Matumizi kwa kazi za kawaida za Shirika ''Management Expenses" ni **TZS 13.7 bilioni;**

ii. Matumizi ya ununuzi wa vitendea kazi kwa matumizi ya watendaji wa Shirika ni **TZS 4.3 bilioni**, ikijumisha ununuzi wa samani za ofisi, ununuzi wa vifaa mbalimbali vya TEHAMA (CT Equipments), pamoja na ununuzi wa magari mawili mapya kwa matumizi ya ofisi za Shirka;

iii. Matumizi ya malipo ya madai kwa wateja watakaoathirika na majanga mbalimbali ya ajali **TZS 13.6 bilioni;** na

iv. Matumizi ya malipo ya ujira kwa mawakala na madalali wanaofanya kazi ya kuuza Bima kwa niaba ya Shirika **TZS 8.5 bilioni.**

**Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT)**

**Mapato**

**127. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, ZIAAT inatarajia kukusanya **TZS 0.608 bilioni** kutoka kwenye vianzio vyake vya mapato ambavyo ni Ada ya Usajili, Utambuzi, Leseni, Uanachama na Ada ya Mafunzo.

### Matumizi

**128. Mheshimiwa Spika,** Katika kuyafikia malengo yaliyowekwa na Taasisi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, ZIAAT imepangiwa kutumia **TZS 2.492 bilioni** ambayo ni ruzuku kutoka Serikalini. Kati ya fedha hizo, **TZS 0.418 bilioni** kwa ajili ya Mishahara na **TZS 2.074 bilioni** kwa kazi za Uendeshaji wa Ofisi zikiwemo:-

i. Kuanzisha Mitihani ya Taaluma ya Kodi pamoja na kuandaa program za udhibiti wa ubora kwa ajili ya kutoa "certification" na kuimarisha ubora wa kazi za wanachama;

ii. Kuongeza "credibility" ya Taasisi kimataifa kwa kujiunga na Shirikisho la wahasibu duniani (IFAC), kuanzisha na kuendeleza Mifumo ya Kidigitali;

iii. Kuingiza kada ya Ununuzi katika usimamizi;na

iv. Kuendeleza mashirikiano na taasisi nyingine ikiwemo NBAA na TCU

### Kampuni ya Zanzibar Treasury Sukuk 1 Limited

**129. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango katika kutekeleza moja ya jukumu lake inasimamia uanzishwaji wa mpango wa SUKUK ya Zanzibar, ambayo ni Hati Fungani ya kwanza inayofuata Misingi ya Shariah kutolewa na Serikali ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Hii ni hatua ya kihistoria na ya kipekee kwa Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali za kubuni mbinu bunifu za kufadhili miradi ya maendeleo.

**130. Mheshimiwa Spika,** Kampuni hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imepangiwa **TZS 0.650 bilioni** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikali ili kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i. Kuweka Mfumo Madhubuti wa Kusimamia Muamala wa SUKUK kwa Kuanzisha na kuendesha mifumo ya kiutawala, kisheria

na kifedha kwa ajili ya kuhakikisha usimamizi bora na wenye ufanisi wa mchakato mzima wa SUKUK ikiwemo ulipaji wa faida za wawekezaji;

ii. Uratibu wa Utoaji wa Sukuk Sokoni kwa Awamu zilizobaki, hivyo Taasisi itasimamia hatua zote za maandalizi na uuzaji wa Hati Fungani kwa wawekezaji kupitia masoko ya mitaji ya ndani na ya kimataifa kwa awamu zilizobaki; na

iii. Kuratibu Vikao vya Wadau Wote wa Sukuk kwa Kuandaa na kuratibu mikutano ya ushauriano na tathmini inayowahusisha wadau wote muhimu wa mpango wa Sukuk.

**Chuo cha Usimamizi wa Fedha (ZIFA)**

**131. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imeanza maandalizi ya kutunga Sheria ya kukianzisha Chuo Cha Usimamizi wa Fedha ambacho kitasimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi imekipangia Ruzuku ya **TZS 0.915 bilioni** kwa ajili ya uendeshaji wa chuo kwa kutekeleza Mikakati ifuatayo:-

i. Kukamilisha Sheria na nyaraka muhimu ili iweze kufanya kazi zake kwa umahiri;

ii. Kupitia mitaala ya mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na kuandaa mitaala ya kozi mpya pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

iii. Kuongeza idadi ya udahili wa Wanafunzi na kufikia 1000;

iv. Kuajiri Wafanyakazi 80, kati yao 50 wahadhiri na 30 wasaidizi (supporting Staffs) kwa lengo la kuzalisha wahitimu wanaoweza kushindana Kimataifa kupitia program bora zitakazotolewa; na

v. Kufanya matangazo mbali mbali pamoja na uwelewa wa Chuo ndani na nje ya Zanzibar.

132. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Taasisi tunazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango inatarajia kusimamia uendeshaji wa taasisi mpya na mifuko kama ifuatayo:-

i. Soko la Mitaji la Zanzibar (Zanzibar Securities Exchange);

ii. Taasisi ya Usimamizi wa Uchumi Halal Zanzibar (Zanzibar Halal Bureau);

iii. Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Maji Zanzibar; na

iv. Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Zanzibar.

133. **Mheshimiwa Spika,** Aidha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (Zanzibar Health Services Fund) utatoka kusimamiwa na Wizara ya Afya na utasimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji wa karibu wa huduma zinazotolewa na Mfuko pamoja na ufuatiliaji wa vyanzo mbadala vya fedha zitakazilipia huduma ya afya.

**Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

134. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango inawaomba wajumbe wa Baraza lako kupokea, kujadili na hatimae kuikubali taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025. Mheshimiwa Spika, ili Ofisi iweze kutekeleza kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 naliomba Baraza lako kuidhinisha Makadirio ya kukusanya Mapato ya **TZS 6,527.599 bilioni** kutokana na vyanzo vya mafungu ya F01, F04, F05 na F07. Aidha kutumia **TZS 1,571.151 bilioni** ili kufanikisha shughuli ilizojipangia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa mafungu F01 mpaka F07 ikiwa ni matumizi ya mishahara, miradi ya maendeleo, matumizi mengineyo pamoja na ruzuku.

## HITIMISHO:

135. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine naomba kutoa shukran zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika, wenyeviti wa Baraza pamoja na Kamati ya Bajeti kwa ushauri, miongozo na mashirikiano mliyotupatia katika kipindi hiki.

136. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango inatoa shukran kwa wadau wote wakiwemo taasisi za serikali, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na wananchi wote kwa ushirikiano wao kwa ofisi yetu.

137. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Dkt. SAADA MKUYA SALUM,**
**WAZIRI WA NCHI-OFISI YA RAIS,**
**FEDHA NA MIPANGO**
**ZANZIBAR**

# VIAMBATANISHO

## VIAMBATANISHO:

## JADWELI 1: MUHTASARI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI, 2024/25

| VIAZIO | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO JULAI - MACHI 2024/2025 | UTEKELEZAJI HALISI JULAI -MACHI 2024/2025 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI JULAI - MACHI 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|
| **MAPATO FO1** | | | | |
| **MAPATO YA KODI** | | | | |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 600,082,000,000 | 300,950,615,075 | 473,318,794,967 | 157 |
| ZRA | 845,979,000,000 | 657,814,683,532 | 667,778,678,116 | 102 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,446,061,000,000** | **958,765,298,607** | **1,141,097,473,083** | 119 |
| MIKOPO NA MISAADA KUTOKA KWA WASHIRIKA WA MAENDELEO | 1,416,517,992,000 | 711,507,757,131 | 277,373,819,928 | 39 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,416,517,992,000** | **711,507,757,131** | **277,373,819,928** | 39 |
| **MAPATO YASIO KUWA YA KODI** | | | | |
| UHAMIAJI | 92,500,000,000 | 82,000,000,000 | 73,814,173,288 | 90 |
| UNUNUZI WA MAGARI | 25,000,000,000 | 18,800,000,000 | 7,745,830,724 | 41 |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI | 15,750,000 | 12,050,000 | 15,450,000 | 128 |
| ADA YA MATUMIZI YA NYARAKA | 457,000,000 | 342,750,000 | 210,407,276 | 61 |
| MATANGAZO | 150,000,000 | 125,000,000 | 7,525,000 | 6 |
| USAJILI WA WAZABUNI | 300,000,000 | 200,000,000 | 216,161,105 | 108 |
| ADA YA MAFUNZO | 82,000,000 | 50,500,000 | 12,330,000 | 24 |
| **JUMLA NDOGO** | **118,504,750,000** | **101,530,300,000** | **82,021,877,393** | **81** |
| **JUMLA FO1** | **2,981,083,742,000** | **1,771,803,355,738** | **1,500,493,170,404** | **85** |
| | | | | |
| **MAPATO FO4** | | | | |
| VIBALI VYA UTAFITI | 78,650,000 | 50,378,500 | 37,353,431 | 74 |
| UKODISHWAJI WA KUMBI ZA MIKUTANO | 20,000,000 | 32,550,000 | 25,850,000 | 79 |
| KUTOA USHAURI ELEKEZI JUU YA MASUALA YA TAFITI | 35,258,000 | 14,458,500 | | - |
| **JUMLA FO4** | **133,908,000** | **97,387,000** | **63,203,431** | **65** |
| | | | | |
| **MAPATO FO5** | | | | |
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI (PAYE) | 21,000,000,000 | 15,750,000,000 | 15,750,000,000 | 100 |
| MABUKU NA STAKABADHI | 30,000,000 | 22,000,000 | 11,457,600 | 52 |
| MCHANGO KUTOKA TAASISI ZA SERIKALI | 31,979,180,000 | 24,321,100,000 | 13,841,775,673 | 57 |
| ADA YA MASOKO | 6,005,500,000 | 4,504,125,000 | 0 | - |
| HATI FUNGANI | 180,000,000,000 | 180,000,000,000 | 179,770,158,547 | 100 |
| MKOPO KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO | 1,532,000,000,000 | 1,087,000,000,000 | 237,900,000,000 | 22 |
| GAWIO LA BOT | 13,500,000,000 | 13,500,000,000 | 13,500,000,000 | 100 |
| MISAADA YA KIBAJETI (GBS/URT) | 100,000,000,000 | 87,000,000,000 | 76,578,263,222 | 88 |
| **JUMLA F05** | **1,884,514,680,000** | **1,412,097,225,000** | **537,351,655,042** | **38** |
| | | | | |
| **MAPATO FO7** | | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 33,701,170,000 | 10,000,000,000 | 8,000,000,000 | 80 |
| KODI YA BOHARI | 470,000,000 | 270,000,000 | 170,456,000 | 63 |
| UUZAJI WA VIFAA VIKONGWE | 1,365,012,000 | 1,023,734,994 | 674,785,000 | 66 |
| KODI ZA MAJENGO ZINAZOSIMAMIWA NA ORFM | 422,830,000 | 413,317,500 | 26,231,000 | 6 |
| **JUMLA FO7** | **35,959,012,000** | **11,707,052,494** | **8,871,472,000** | **76** |
| | | | | |
| **JUMLA KUU** | **4,901,691,342,000** | **3,195,705,020,232** | **2,046,779,500,877** | **64** |

**JADWELI 2: MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO JULAI-MACHI, 2024/25 (TARAKIMU NI TZS MILLIONI)**

| Program u Kuu | Programu ndogo | Makisio Mwaka (2024-2025) | Makisio Julai-Machi( 2024-2025) | Mishahara | Matumizi Menginejo | Miradi ya Maendeleo | | Ruzuku | Jumla | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Julai-Machi 2024-2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | SMZ | Mhisani | | | |
| Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma | Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | 1,313.19 | 1,116.21 | 640.45 | 294.33 | | | | 934.78 | 84 |
| | Marekebisho ya Mishahara | 130,665.10 | 97,998.82 | 29,569.20 | | | | | 29,569.20 | 30 |
| | Uratibu wa Fedha za Nje | 848.37 | 687.59 | 232.90 | 89.57 | | | | 322.47 | 47 |
| | Fedha na Sera za Kodi | 28,928.87 | 21,630.95 | 244.66 | 58.23 | | | 20,654.85 | 20,957.74 | 97 |
| | **Jumla ndogo** | **161,755.53** | **121,433.57** | **30,687.21** | **442.13** | | | **20,654.85** | **51,784.19** | **43** |
| Usimamizi wa Sera za Manunuzi na Masuala ya Shena | Usimamizi wa Sera za Manunuzi | 4,080.03 | 3,495.78 | 407.49 | 56.76 | | | 1,565.54 | 2,029.79 | 58 |
| | Usimamizi wa Huduma za Kishera za Ofisi ya Rais - Rais Fedha na Mipango | 358.66 | 265.69 | | 88.97 | | | | 88.97 | 33 |
| | **Jumla ndogo** | **4,438.69** | **3,761.47** | **407.49** | **145.73** | | | **1,565.54** | **2,118.76** | **56** |
| Uendeshaji na uratibu wa wizara ya Fedha na Mipango | Utumishi na Uendeshaji | 32,390.04 | 29,984.82 | 1,404.90 | 25,579.92 | | | | 26,984.82 | 90 |
| | Mipango, Sera na Utafiti | 464,380.49 | 250,416.37 | 200.60 | 21.51 | 177,669.11 | 17,193.22 | | 195,084.44 | 78 |
| | Ofisi kuu Pemba | 2,428.21 | 1,948.19 | 462.09 | 377.74 | | | | 839.83 | 43 |
| | **Jumla ndogo** | **499,198.74** | **282,349.38** | **2,067.59** | **25,979.17** | **177,669.11** | **17,193.22** | | **222,909.10** | **79** |
| | **Jumla F01** | **665,392.96** | **407,544.42** | **33,162.29** | **26,567.03** | **177,669.11** | **17,193.22** | **22,220.39** | **276,812.04** | **68** |
| Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | 416,897.40 | 323,861.73 | 2,206.97 | 282,395.60 | | | | 284,602.57 | 88 |
| | **Jumla ndogo** | **416,897.40** | **323,861.73** | **2,206.97** | **282,395.60** | | | | **284,602.57** | **88** |
| | **Jumla F02** | **416,897.40** | **323,861.73** | **2,206.97** | **282,395.60** | | | | **284,602.57** | **88** |
| Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi | Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini | 3,473.30 | 3,303.820 | 153.27 | 162.07 | 2,264.96 | | | 2,580.30 | 78 |
| | Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu | 982.26 | 829.445 | 185.14 | 80.80 | | | | 265.94 | 32 |
| | Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo | 2,924.90 | 2,546.930 | 291.15 | 108.67 | 439.60 | | | 839.42 | 33 |
| | **Jumla Ndogo** | **7,380.46** | **6,680.19** | **629.57** | **351.53** | **2,704.56** | | | **3,685.66** | **55** |
| Usimamizi wa Uchumi Mkuu | Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu | 593.30 | 455.822 | 202.23 | 90.67 | | | | 292.89 | 64 |
| | Utafiti na Ubunifu | 991.48 | 814.355 | 153.69 | 252.99 | | | | 406.68 | 50 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,584.78** | **1,270.18** | **355.92** | **343.66** | | | | **699.57** | **55** |
| Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango. | 2,278.99 | 1,776.129 | 517.67 | 746.71 | | | | 1,264.38 | 71 |
| | Uratibu wa Shughuli za Tume ya Mipango Pemba | 522.34 | 398.901 | 254.87 | 77.51 | | | | 332.38 | 83 |
| | **Jumla Ndogo** | **2,801.33** | **2,175.03** | **772.54** | **824.22** | | | | **1,596.76** | **73** |
| | **Jumla F03** | **11,766.57** | **10,125.40** | **1,758.03** | **1,519.41** | **2,704.56** | | | **5,981.99** | **59** |

Inaendelea chini …..

| Programu Kuu | Programu ndogo | Makisio Mwaka (2024-2025) | Makisio Julai-Machi( 2024-2025) | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Miradi ya Maendeleo | | Ruzuku | Jumla | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Julai-Machi 2024-2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | SMZ | Mhisani | | | |
| Kuendeleza na kuratibu Takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii | Ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii | 7,314.85 | 5,501.75 | 792.04 | 156.77 | | 2,802.06 | | 3,750.87 | 68 |
| | Uratibu wa shughuli za Kitakwimu katika mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar | 1,581.77 | 1,175.10 | 208.40 | 63.52 | | 615.69 | | 887.62 | 76 |
| | **Jumla ndogo** | **8,896.61** | **6,676.85** | **1,000.44** | **220.29** | | **3,417.75** | | **4,638.49** | **69** |
| Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | Utawala na Uendeshaji Unguja | 3,742.21 | 2,849.41 | 513.61 | 167.60 | | 255.44 | | 936.65 | 33 |
| | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Takwimu Pemba | 474.75 | 357.65 | 248.56 | 54.59 | | | | 303.15 | 85 |
| | **Jumla ndogo** | **4,216.96** | **3,207.06** | **762.17** | **222.19** | | **255.44** | | **1,239.80** | **39** |
| | **Jumla F04** | **13,113.57** | **9,883.91** | **1,762.61** | **442.49** | | **3,673.19** | | **5,878.29** | **59** |
| Usimammizi wa Hazina | Ufuatiliaji wa Mapato ya Serikali yasiyokuwa ya Kodi | 58.36 | 39.08 | | 7.33 | | | | 7.33 | 19 |
| | Kusimamia ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali | 213.38 | 126.60 | | 115.71 | | | | 115.71 | 91 |
| | Usimamizi wa Matumizi ya Serikali | 552.53 | 345.08 | | 137.89 | | | | 137.89 | 40 |
| | Usumamizi wa Deni la Taifa | 266.12 | 100.52 | | 109.20 | | | | 109.20 | 109 |
| | **Jumla ndogo** | **1,090.39** | **611.28** | | **370.13** | | | | **370.13** | **61** |
| Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Uratibu wa Mipango | 101.17 | 79.16 | | 23.32 | | | | 23.32 | 29 |
| | Utawala na Uendeshaji Unguja | 10,308.09 | 7,611.85 | 6,387.91 | 401.62 | | | | 6,789.53 | 89 |
| | Utawala na Uendeshaji Pemba | 3,254.36 | 2,347.01 | 2,187.61 | 184.17 | | | | 2,371.78 | 101 |
| | **Jumla ndogo** | **13,663.62** | **10,038.02** | **8,575.52** | **585.79** | | | | **9,184.63** | **91** |
| | **Jumla F05** | **14,754.01** | **10,649.30** | **8,575.52** | **955.92** | | | | **9,554.76** | **90** |
| Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikali | Usimamizi wa kamati za Ukaguzi na Taarifa jumuishi za ukaguzi wa ndani | 142.115 | 116.89 | - | 32.57 | | | | 32.568 | 28 |
| | Uchunguzi wa Ubadhirifu na vihatarishi | 397.84 | 361.34 | | 82.87 | | | | 82.868 | 23 |
| | Usimamizi wa uthibitisho wa ubora | 285.34 | 274.45 | | 45.037 | | | | 45.037 | 16 |
| | **Jumla ndogo** | **825.29** | **752.67** | | **160.47** | | | | **160.47** | **21** |
| Utawala na Uendeshaji | Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango,Mafunzo na Utafiti | 4,154.20 | 3,222.84 | 2,540.57 | 360.86 | | | | 2,901.43 | 90 |
| | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Ofisi Pemba | 1,090.01 | 844.00 | 615.91 | 91.36 | | | | 707.27 | 84 |
| | **Jumla ndogo** | **5,244.21** | **4,066.84** | **615.91** | **452.22** | | | | **3,608.69** | **89** |
| | **Jumla F06** | **6,069.50** | **4,819.51** | **615.91** | **612.69** | | | | **3,769.17** | **78** |
| Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma | Usimamizi wa mali za Umma | 2,625.34 | 1,981.79 | | 860.64 | | | | 860.64 | 43 |
| | Uwekezaji wa Mashirika ya Umma | 642.64 | 491.47 | | 131.33 | | | | 131.33 | 27 |
| | **Jumla ndogo** | **3,267.98** | **2,473.25** | | **991.96** | | | | **991.96** | **40** |
| Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina | Usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,342.90 | 1,017.60 | 611.03 | 691.42 | | | | 1,302.45 | 128 |
| | Uratibu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Pemba | 608.50 | 450.86 | 129.66 | 137.73 | | | | 267.39 | 59 |
| | **Jumla ndogo** | **1,951.39** | **1,468.46** | **740.69** | **829.15** | | | | **1,569.84** | **107** |
| | **Jumla F07** | **5,219.37** | **3,941.71** | **740.69** | **1,821.12** | | | | **2,561.80** | **65** |
| | **JUMLA KUU F01+F02+F03+F04+ F05+F06+F07** | **1,133,213.37** | **770,825.98** | **48,822.02** | **314,314.25** | **180,373.67** | **20,866.41** | **22,220.39** | **589,160.63** | **76** |

## JADWELI 3: MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

| VIANZIO | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2025/2026 | ASILIMIA YA ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| **MAPATO FO1** | | | |
| **MAPATO YA KODI** | | | |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 600,082,000,000.00 | 825,769,572,000.00 | 38 |
| ZRA | 845,979,000,000.00 | 1,257,240,356,000.00 | 49 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,446,061,000,000.00** | **2,083,009,928,000.00** | **44** |
| MIKOPO NA MISAADA KUTOKA KWA WASHIRIKA WA MAENDELEO | 1,416,517,992,000.00 | 1,324,841,519,000.00 | -6 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,416,517,992,000.00** | **1,324,841,519,000.00** | **-6** |
| **MAPATO YASIOKUWA YA KODI** | | | |
| UHAMIAJI | 92,500,000,000.00 | 104,578,439,000.00 | 13 |
| UNUNUZI WA MAGARI | 25,000,000,000.00 | 5,000,000,000.00 | -80 |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI | 15,750,000.00 | 25,000,000.00 | 59 |
| ADA YA MATUMIZI YA NYARAKA | 457,000,000.00 | 548,000,000.00 | 20 |
| MATANGAZO | 150,000,000.00 | 165,000,000.00 | 10 |
| USAJILI WA WAZABUNI | 300,000,000.00 | 360,000,000.00 | 20 |
| ADA YA MAFUNZO | 82,000,000.00 | 102,000,000.00 | 24 |
| **JUMLA NDOGO** | **118,504,750,000.00** | **110,778,439,000.00** | **-7** |
| **JUMLA FO1** | **2,981,083,742,000.00** | **3,518,629,886,000.00** | **18** |
| **MAPATO FO4** | | | |
| VIBALI VYA UTAFITI | 78,650,000.00 | 105,842,000.00 | 35 |
| UKODISHWAJI WA KUMBI ZA MIKUTANO | 20,000,000.00 | 47,602,000.00 | 138 |
| KUTOA USHAURI ELEKEZI JUU YA MASUALA YA TAFITI | 35,258,000.00 | 26,866,000.00 | -24 |
| **JUMLA F04** | **133,908,000.00** | **180,310,000.00** | **35** |
| **MAPATO FO5** | | | |
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI (PAYE) | 21,000,000,000.00 | 21,000,000,000.00 | 0 |
| MCHANGO MAMLAKA(ZURA) | 10,000,000,000.00 | 10,000,000,000.00 | 0 |
| MABUKU NA STAKABADHI | 30,000,000.00 | 30,000,000.00 | 0 |
| MCHANGO KUTOKA TAASISI YA VIWANGO (ZBS) | 2,500,000,000.00 | 2,500,000,000.00 | 0 |
| MCHANGO KUTOKA BPRA | 480,000,000.00 | 480,000,000.00 | 0 |
| MCHANGO KUTOKA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI | 2,000,000,000.00 | 2,000,000,000.00 | 0 |
| MCHANGO KUTOKA KAMISHENI YA UTALII | 5,000,000,000.00 | 5,000,000,000.00 | 0 |
| HATI FUNGANI | 180,000,000,000.00 | 1,080,000,000,000.00 | 500 |
| MKOPO KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO | 1,532,000,000,000.00 | 1,700,000,000,000.00 | 11 |
| GAWIO LA BOT | 13,500,000,000.00 | 13,500,000,000.00 | 0 |
| MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA) | 2,500,000,000.00 | 2,500,000,000.00 | 0 |
| MAMLAKA YA MAJI (ZAWA) | 3,750,000,000.00 | 3,750,000,000.00 | 0 |
| MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) | 2,225,000,000.00 | 2,225,000,000.00 | 0 |
| KAMISHENI YA ARDHI | 3,524,180,000.00 | 3,524,180,000.00 | 0 |
| MISAADA YA KIBAJETI (GBS/URT) | 100,000,000,000.00 | 120,000,000,000.00 | 20 |
| MAPATO YATOKANAYO NA UENDESHAJI WA MASOKO | 6,005,500,000.00 | 6,000,000,000.00 | -0 |
| RIBA YA AMANA | * | 7,280,000,000.00 | 0 |
| MCHANGO KUTOKA ZFDA | * | 500,000,000.00 | 0 |
| **JUMLA F05** | **1,884,514,680,000.00** | **2,980,289,180,000.00** | **58** |
| **MAPATO FO7** | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 33,701,170,000.00 | 25,059,300,000.00 | -26 |
| KODI YA BOHARI | 470,000,000.00 | 500,000,000.00 | 6 |
| UUZAJI WA VIFAA VIKONGWE | 1,365,012,000.00 | 2,400,000,000.00 | 76 |
| KODI YA MAJENGO ZINAZOSIMAMIWA NA ORFM | 422,830,000.00 | 325,000,000.00 | -23 |
| MAPATO YA MASHAMBA | ** | 215,700,000.00 | 0 |
| **JUMLA F07** | **35,959,012,000.00** | **28,500,000,000.00** | **-21** |
| **JUMLA KUU** | **4,901,691,342,000.00** | **6,527,599,376,000.00** | **33** |

Angalizo

(*): Mapato ya Riba ya Amana na Mchango kutoka ZFDA yataanzwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

kutokuwepo kwa michango ya fedha za ununuzi wa magari ambapo mwaka jana fedha nyingi zilibeba mchango wa magari makubwa ya ZECO ambayo tayari yamesha nunuliwa

(**) Mapato ya Mashamba yataanzwa kukusanywa 2025/2026

## JADWELI 4: MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 (TARAKIMU NI TZS MILLIONI)

| Programu Kuu | Programu ndogo | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Miradi ya Maendeleo | | Ruzuku | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | Mhisani | | |
| Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma | Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | 835.18 | 1,284.42 | | | | 2,119.60 |
| | Marekebisho ya Mishahara | 99,904.87 | | | | | 99,904.87 |
| | Uratibu wa Fedha za Nje | 309.01 | 526.47 | | 276.15 | | 1,111.63 |
| | Fedha na Sera za Kodi | 330.37 | 1,276.33 | | | 33,602.90 | 35,209.60 |
| | **Jumla ndogo** | **101379.427** | **3087.22** | | **276.15** | **33602.9** | **138345.697** |
| Usimamizi wa Sera za Manunuzi na Masuala ya Sheria | Usimamizi wa Sera za Ununuzi | 538.47 | 268.44 | | | 3,274.20 | 4,081.11 |
| | Huduma za Kisheria za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | | 472.65 | | | | 472.65 |
| | **Jumla ndogo** | **538.47** | **741.09** | | | **3274.2** | **4553.76** |
| Uendeshaji na uratibu wa wizara ya Fedha na Mipango | Utumishi na Uendeshaji | 2,325.00 | 30,996.71 | | | | 33,321.71 |
| | Mipango, Sera na Utafiti | 268.06 | 484.18 | 649,098.32 | 36,900.00 | | 686,750.56 |
| | Ofisi kuu Pemba | 594.81 | 2,568.00 | | | | 3,162.81 |
| | **Jumla ndogo** | **3187.87** | **34048.887** | **649098.32** | **36900** | | **723235.077** |
| | **Jumla F01** | **105,105.767** | **37,877.197** | **649,098.320** | **37,176.150** | **36,877.100** | **866,134.534** |
| Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | 3,013.20 | 638,337.100 | | | | 641,350.30 |
| | **Jumla ndogo** | **3013.2** | **638337.1** | | | | **641350.3** |
| | **Jumla F02** | **3,013.200** | **#######** | | | | **641,350.300** |
| Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya watendakazi | Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini | 217.14 | 482.229 | 10,000.00 | | | 10,699.368 |
| | Maendeleo ya Watendakazi wa Masuala ya Idadi ya Watu | 265.24 | 1,076.891 | | | | 1,342.133 |
| | Mipango ya Maendeleo | 411.97 | 533.351 | 1,800.000 | | | 2,745.322 |
| | **Jumla ndogo** | **894.35143** | **2092.47157** | **11800** | | | **14786.823** |
| Usimamizi wa Uchumi Mkuu | Usimamizi wa Uchumi Mkuu | 281.93 | 456.222 | | | | 738.148 |
| | Utafiti | 220.96 | 597.403 | 1,000.00 | | | 1,818.358 |
| | **Jumla ndogo** | **502.88** | **1,053.62** | **1,000.00** | | | **2,556.51** |
| Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | 745.37 | 1,469.114 | | | | 2,214.487 |
| | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Pemba | 353.69 | 469.100 | | | | 822.794 |
| | **Jumla ndogo** | **1099.067262** | **1938.213738** | | | | **3037.281** |
| | **Jumla F03** | **2,496.300** | **5,084.310** | **12,800.000** | | | **20,380.610** |

Inaendelea chini ……

| Programu Kuu | Programu ndogo | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Miradi ya Maendeleo | | Ruzuku | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | Mhisani | | |
| Kuendeleza na kuratibu Takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii | Ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii | 1,149.81 | 859.07 | 320.00 | 4,479.90 | | 6,808.784 |
| | Uratibu wa shughuli za Kitakwimu katika mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar | 308.95 | 229.140 | | 846.07 | | 1,384.160 |
| | **Jumla ndogo** | **1458.76** | **1088.214** | **320** | **5325.97** | | **8192.944** |
| uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | Utawala na Uendeshaji Unguja | 697.29 | 959.484 | | 1,272.80 | | 2,929.574 |
| | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Takwimu Pemba | 329.75 | 155.00 | | | | 484.751 |
| | **Jumla ndogo** | **1027.039** | **1114.486** | | **1272.8** | | **3414.325** |
| | **Jumla F04** | **2,485.799** | **2,202.700** | **320.000** | **6,598.770** | | **11,607.269** |
| Usimamizi wa Hazina | Ufuatiliaji wa Mapato Yasiyokuwa ya Kodi | | 46.864 | | | | 46.864 |
| | Kusimamia Ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali | | 112.235 | 1,023.875 | | | 1,136.110 |
| | Usimamizi wa Matumzi ya Serikali | | 582.080 | | | | 582.080 |
| | Usumamizi wa Deni la Taifa | | 313.980 | | | 650.300 | 964.280 |
| | **Jumla ndogo** | | **1055.159** | **1023.875** | | **650.3** | **2729.334** |
| Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Uratibu wa Mipango | | 236.835 | | | | 236.835 |
| | Utawala na Uendeshaji Unguja | 9,240.145 | 1,803.306 | | | | 11,043.451 |
| | Utawala na Uendeshaji Pemba | 3,129.955 | 449.800 | | | | 3,579.755 |
| | **Jumla ndogo** | **12370.1** | **2489.941** | | | | **14860.041** |
| | **Jumla F05** | **12,370.100** | **3,545.100** | **1,023.875** | | **650.300** | **17,589.375** |
| Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini | Usimamizi wa kamati za Ukaguzi na Taarifa jumuishi za ukaguzi wa ndani | | 122.180 | | | | 122.180 |
| | Uchunguzi wa Ubadhirifu na vihatarishi | | 459.823 | | | | 459.823 |
| | Usimamizi wa uthibitisho wa ubora | | 619.080 | | | | 619.080 |
| | **Jumla ndogo** | | **1201.083** | | | | **1201.083** |
| Utawala na Uendeshaji | Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango,Mafunzo na Utafiti | 3,615.81 | 582.74 | | | | 4,198.55 |
| | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Ofisi Pemba | 865.39 | 214.47 | | | | 1,079.86 |
| | **Jumla ndogo** | **4481.2** | **797.212** | | | | **5278.412** |
| | **Jumla F06** | **4,481.200** | **1,998.295** | | | | **6,479.495** |
| Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma | Usimamizi wa mali za Umma | | 385.60 | | | | 385.600 |
| | Uwekezaji wa Mashirika ya Umma | | 3,759.17 | | | | 3,759.165 |
| | **Jumla ndogo** | | **4144.765** | | | | **4144.765** |
| Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina | Usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina | 856.64 | 2,166.05 | | | | 3,022.692 |
| | Uratibu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Pemba | 256.26 | 185.89 | | | | 442.143 |
| | **Jumla ndogo** | **1112.9** | **2351.935** | | | | **3464.835** |
| | **Jumla F07** | **1,112.900** | **6,496.700** | | | | **7,609.600** |
| **JUMLA KUU F01+F02+F03+F04+F05+F06+F07** | | **131,065.266** | **695,541.402** | **663,242.195** | **43,774.920** | **37,527.400** | **1,571,151.183** |

## JADWELI 5: MAPENDEKEZO YA MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (TARAKIMU NI TZS MILIONI)

| S/N | PROGRAMU/ MIRADI | WASHIRIKA WA MAENDELEO | FEDHA ZA SMZ | MKOPO | MISAADA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Fungu F01** | | | | | |
| 1 | **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | | | | |
| | Ukamilishwaji wa Ofisi za Serikali | | 59,576.41 | | | 59,576.41 |
| | Ujenzi wa Mji wa Serikali | | 66,722.16 | | | 66,722.16 |
| 2 | Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha ( PFMRP) | Benki ya Dunia | 350.00 | 4,400.00 | | 4,750.00 |
| 3 | Uimarishaji wa Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISPDRM) | | 50.00 | | | 50.00 |
| 4 | Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar ( BIG-Z) | | | 32,500.00 | | 32,500.00 |
| 5 | Ulipaji wa Madeni kwa Miradi ya Maendeleo | | 312,000.00 | | | 312,000.00 |
| 6 | Ulipaji wa Fidia za Miradi ya Maendeleo | | 210,399.75 | | | 210,399.75 |
| 7 | Mradi wa Msaada wa kiufundi kwa ajili ya kukuza uwezo wa uhamasishaji utafutaji rasilimali Fedha | | | | 276.15 | 276.15 |
| | **Jumla Ndogo(F01)** | | **649,098.32** | **36,900.00** | **276.15** | **686,274.47** |
| | **Fungu F03** | | | | | |
| 6 | Mradi wa Mapitio, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini wa Mpango wa maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, VISION 2050, SDGs na AFRICAN AGENDA) | | 1,800.00 | | | 1,800.00 |
| 7 | Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo | | 5,500.00 | | | 5,500.00 |
| 8 | Kuratibu Mpango wa Kurasimisha Ardhi na Biashara Zanzibar | | 4,500.00 | | | 4,500.00 |
| | Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati kwa Fedha za Ndani SMZ | | 1,000.00 | | | 1,000.00 |
| | **Jumla Ndogo(F3)** | | **12,800.00** | | | **12,800.00** |
| | **Fungu F04** | | | | | |
| 9 | Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) | Benki ya Dunia | | 4,598.77 | | 4,598.77 |
| 10 | Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za jinsia | UN -Women | 2,000.00 | 320.00 | | 320.00 |
| | **Jumla Ndogo (F04)** | | **2,000.00** | **6,598.77** | | **6,918.77** |
| | **Fungu F05** | | | | | |
| 11 | Utekelezaji wa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu (IPSAS ACCRUAL) | | 1,023.88 | | | 1,023.88 |
| | **Jumla Ndogo (F05)** | | **1,023.88** | | | **1,023.88** |
| | **JUMLA KUU( F01+F03+F04+ F05)** | | **664,922.20** | **707,017.12** | **276.15** | **707,017.12** |